# *Hukumu Kwa Uwakilishi*

Asante, Ndugu Orman . . . ? . . .

Ni vizuri sana kuwa kanisani tena, asubuhi hii, na kuwa na wakati huu wa ushirika kwenye mambo haya makuu ya Mungu. Na sasa, kamwe hatuna haraka hapa kwenye maskani, mwajua. Kwa namna fulani sisi huchukua muda wetu, na wakati mwingine kidogo inachosha kwa wale waliosimama. Na kadiri wawezavyo, ama wanavyoweza, hutoka nje wakati mwingine na kutoa . . . Ikiwa mtu fulani, watoto, wangetaka kuja karibu zaidi kidogo hapa, nafikiri tunaweza kuwapa nafasi wengine wachache.

2 Na hivi hapa viti viwili zaidi, vitatu, yapata vinne, hapa juu kwenye jukwaa, ikiwa mtu yeyote huko nyuma angetaka kuja hapa juu na astarehe, ama kama mtu kidogo yuko nyuma, ikiwa ni mara yao ya kwanza kanisani na baadhi ya wazee wangekuja hapa juu na kuketi, tungefurahia kuwa nao hapa juu, kusudi mtu mwingine apate kiti. Baadhi ya mashemasi, ama— ama mhudumu fulani, ama kadhalika, ambaye angeweza kuja hapa juu, huenda ikawa ni fursa ya kumpa mtu mwingine ki— kiti, ambaye amesimama. Na baadhi ya watu wangali wanakuja huku, wakijaribu kuingia kwenye nafasi, huko nyuma. Wanaona marefu yamefungwa, kisha wanaondoka na kukosa.

3 Sasa, hiki hapa kiti cha ziada hapa juu, mbele, naamini. Hiyo ni kweli, msichana? Papa hapa kuna kiti hapa, moja kwa moja mbele, papa hapa. Pia ninamwona Ndugu Wood anasimama. Vipo viwili zaidi hapa juu. Endeleeni tu kupanda juu huku. Viwili zaidi, papa hapa mbele. Kama mtu yeyote anataka kuja mbele, kiko kiti kimoja, viwili, vitatu, viti vitatu viko tupu hapa, labda vinne, hapa jukwaani. Nanyi mtakuja huku juu, vema, basi, hiyo itafungua nafasi ya viti vingine huko nyuma.

4 Maana, mara nyingi, watu wanaingia, baada ya ibada kuanza. Wataangalia kote, kwenye mlango wa nyuma, kisha warudi nyuma tena. Na wanakosa ibada.

5 Hiki hapa kimoja hapa, kimoja moja kwa moja katikati. Naam. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Hiyo inafanya viti vitano vitupu sasa, hapa mbele. Wewe njoo moja kwa moja huku, ujisikie huru na kukaribishwa. Bwana akubariki, Ndugu George. Nina furaha kukuona tena asubuhi ya leo. Huku ninii . . . Hilo ni jema sana.

6 Dada, sasa, wewe, msichana mdogo, ikiwa yeye . . . Kipo kimoja moja kwa moja huko nyuma kwa ajili yake. Papo hapo, kipenzi. Nenda moja kwa moja pale nyuma ambapo yule mwanamume amesimama. Kwenye . . . Papo hapo. Uh-huh.

7 Hilo ni jema. Kila mtu ameketi starehe, basi wanajisikia vizuri zaidi. Wanajisikia kana kwamba unaweza. . .Ninajua si starehe sana hapa ndani, bali tunawatakeni nyinyi mwe ka—karibu sana tuwezavyo kuwafanya.

8 Sasa, tunatazamia mkutano ujao, tukitarajia baraka kuu siku za usoni, mkutano huu unaokuja wa unabii.

9 Sasa, asubuhi ya leo, niliwaambia jamaa nilikuwa ninaenda kuwaombea wagonjwa. Na hii itakuwa ndiyo nafasi ya mwisho nitakayokuwa nayo sasa, kuwaombea wagonjwa, kanisani, mpaka baada ya mkutano. Kwenye wakati wa mkutano, tunataka kuudumisha kwenye mkondo wa unabii, ikiwa tunaweza. Ndipo, baada ya hapo, nafikiri, labda—labda kabla ya Krismasi, ningetaka labda kuwa na maskini mkutano mwingine wa siku kadhaa usiku juu ya Danieli, hapa kanisani. Kwa sababu, labda mwanzo wa mwaka, nita—nitakuwa ninaondoka tena. Nami ninajua hatuna muda mwingi sana uliosalia.

10 Kwa hivyo, sasa, ikiwa mtu yeyote anakuja na anataka kuwekewa nafasi kwenye moteli, na kadhalika, tumeandaa hiyo sasa, ili tuweze kuwekewa nafasi.

11 Naye Bw. Morris, ambaye aliponywa kansa ya koo, alikuwa ni mwanasarakasi. Alioa katika familia ya Dk. Adair, rafiki yangu hapa mjini, na ambaye alimfanyia upasuaji kwa sababu ya kansa ya koo. Naye alikuwa yuafa. Ndipo Bwana akaniongoza nyumbani kwake, miaka sita, saba iliyopita, ambapo alikuwa amelala kwa dada yake, akifa, kwa kansa ya koo. Ndipo nikamkuta—nikamkuta, hapa juu kwenye duka la kinyozi, hivi majuzi, akishuhudia. Kasema, “Nilikuwa siwezi hata kumeza.” Tena kasema, “Katika dakika tano, baada ya kuombewa, nikala chakula changu cha jioni.” Na akasema hakujawa hata na chembe yake moja tangu wakati huo.

12 Yeye huendesha Wayfare Motel. Ndipo akasema, “Billy, nasikia una mkutano unaokuja. Na yeyote wa watu wako atakayeingia hapa, nitawapa gharama ya chini kuliko yote.” Anayo moteli mpya hapa. “Na kuwapa gharama za jamaa, na—na kadhalika.” Basi nikachukua kadi zake, na ziko ofisini, na kadhalika. Na tunaweza kuwasiliana na kuingia sehemu zingine ambapo sisi. . .baada ya nafasi zilizohifadhiwa kuisha, ambapo tunaweza kupata bei nzuri kuliko zote, nyumba nzuri sana za kupangisha, kukidhi kile wao, rafiki zako, wanachofikiri ni bora zaidi.

13 Wengi wenu, hakika, labda watakuwa na baadhi yao nyumbani kwenu. Na hilo ni jema sana, kama unaweza kumtunza mtu. Ni—ni ya starehe zaidi, kama vile nyumbani, mnajua, unapoweza kuwa na Wakristo, na kufanya ushirika. Na basi kwa namna fulani, mnaweza kwenda, muyapitie Maandiko, pamoja.

14 Ninawatakeni, kila mmoja, kilete kitabu chako, ilete penseli yako. Maana, tutataja nyakati, miaka, Maandiko, juu ya Nyakati Saba za Kanisa, nyakati za kanisa, nyakati saba za mwisho za kanisa na jinsi zinavyolundikana. Nao ni Ujumbe wa kinabii. Baada ya hayo . . . Kwanza, nitaihubiri, kisha inaingia kwenye kanda, kanda ya sumaku; kutoka hapo, inaingia kwenye kumbukumbu; na kisha ina—inachukuliwa kwa hati mkato, na halafu kuchapishwa kuwa kitabu. Navyo vitabu vitakuwa ni maelezo juu ya—juu ya Nyakati Saba za Kanisa.

15 Na kama sikufikiria kuwa ni muhimu, na kama sikufikiria kwamba ilihitajika sana, hakika nisingechukua muda wa watu kulisema. Lakini ninaamini ya kwamba huenda ikawa ndio mara ya mwisho ambapo tutaipokea, kutoka kanisa hili, hasa. Hivyo basi sasa tuwe wenye kuomba sana kuihusu, wenye kuomba sana.

16 Sasa, juma lijalo, inanibidi kwenda Louisiana, mwajua, kwa ajili ya mkutano huko chini. Na nitakuwa huko Shreveport, Louisiana, kuanzia tarehe 24 hadi tarehe 27 mfululizo, huko Shreveport, Louisiana, pamoja na Ndugu Moore. Na hiyo ni ibada ya kawaida tu ya kiinjilisti. Ndipo basi ninarudi hapa tarehe 29 ama 30.

17 Halafu tarehe 4 Desemba tunaanza hapa. Sasa, kutakuwa na Ujumbe wa asubuhi. Na sasa, kama siwezi, wakati wa usiku, kufikisha wakati huo wa kanisa mahali nafikiri unapaswa kuwa, hata watu wauelewe kikamilifu, basi nitapitia moja kwa moja kesho yake asubuhi, ama alasiri inayofuata, niumalize, hapa maskanini. Halafu nirudi kwenye wakati wa kanisa, usiku huo unaofuata, maana ninataka kuwa na hakika kuwa umeeleweka kabisa, mnaona, maana ni wa muhimu.

18 Tunajua kwamba tunaishi katika wa—wakati wa kipekee sana, na sisi—sisi tunajua hilo kwa—kwa jinsi ambavyo mambo yanalundikana. Na sasa katika hili . . . na kile nisemacho kutoka maskanini, kama kuna wageni hapa, sababu ya mimi kuleta Jumbe hizi, na kadhalika, kwenye maskani, na si huko nje katika huduma ya uinjilisti, ni kwa sababu hiki ni kituo chetu cha nyumbani hapa. Na hapa ninajisikia kwamba ninaweza kuhubiri mafundisho jinsi ninavyoyaona, jinsi ninavyoyaamini. Sasa, hilo haligongani na dini ya mtu yeyote. Mnaona? Chochote kile wanachotaka kuamini, hiyo ni sawa. Na sasa kuna mara nyingi . . .

19 Unajua, ikiwa sote tungeenda, asubuhi ya leo, tuchukue alama za vidole, hakuna mmoja wetu hapa tulio na vidole gumba vinavyofana. Wanadai kwamba hakuna pua mbili zinazofanana. Nadhani nyote mna furaha haifanani na yangu. Bali—bali hakuna watu wawili wanaofanana kabisa. Hivyo basi, mambo mawili, basi kumbuka. Ila sote tutakubali na

kukubaliana kwamba tunampenda Bwana Yesu. Juu ya hiyo mi-. . . Nilisema . . .

20 Kama Mkatoliki wa Kirumi, ikiwa anategemea kanisa Katoliki, ambalo ndilo fundisho lao la kimsingi, lakini kama anaamini ya kwamba hilo kanisa Katoliki litamwokoa, amepotea. Lakini ikiwa anamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, na kumtegemea Yeye kwa ajili ya wokovu, ameokoka. Ikiwa Mmethodisti, ama Mpentekoste, ama Mbaptisti, ikiwa wanategemea kanisa lao ama dhehebu lao kuwaokoa, wamepotea. Lakini, ikiwa wanamtegemea Yesu Kristo, na kumkubali Yeye! Kwa sababu, ni imani yako mwenyewe binafsi katika Kristo Yesu inayotuokoa. Kama wewe ni Mbaptisti, Mpentekoste, Mlutheri, Mkatoliki, Myahudi, ama chochote kile, ni imani yako binafsi katika Yesu Kristo. Mimi—mimi . . .

21 Hii ni kanda ya sumaku, pia. Inaenda sasa hivi, kwa hiyo nina hakika kwamba kila mtu anaelewa hilo wazi.

22 Lakini wakati mtu anapohubiri fundisho, basi inakubidi kubakia na imani yako mwenyewe. Usipofanya hivyo, basi wewe ni mnafiki. Ukisema jambo fulani kwa sababu mtu mwingine analisema, na ndani ya moyo wako huamini hilo, basi wewe ni mnafiki, kwa sababu unasema jambo ambalo huliamini. Afadhali ni—nikosolewe kidogo juu ya mambo ambayo ninaamini, kuliko kuwa mnafiki machoni pa Mungu, kwa kujaribu kupatana na mtu mwingine.

23 Basi sasa, juu ya mikutano hii hapa, huenda usikubaliane na baadhi ya mambo haya, kabisa, bali usi—usikosane nami. Maana, mimi . . . ama sababu . . . mimi—mimi—mimi ninawapenda, na hiyo ni kweli.

24 Nafikiri ninaliweka wazi kwamba ninaamini, kila mmoja wenu, kama wewe ni Mkatoliki, Mprotestanti, ama Myahudi, au chochote ulicho, ikiwa unategemea na umemkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi, umeokoka. "Kwa kuwa ni kwa imani tunaokolewa, hiyo—hiyo ni kwa neema." Na hivyo basi makanisa yetu, vema, ushirika wetu wa makanisa, hautafaa kitu.

25 Bali nafikiri, katika hili, kama utakuja na usiwe na upendeleo, kwamba utakuta kuwa dhehebu lilo hilo la kanisa ndilo ambalo limetutenganisha jinsi tulivyo sasa. Hilo ndilo limeleta shida. Unaona? Na laiti tungaliliacha Hilo tu jinsi lilivyokuwa.

26 Sasa, ninaacha kitu fulani hapa. Nami ni—ninataka kutoa nukuu. Pia nina hakika ya kwamba nyinyi hapa, wa maskanini, rafiki zangu, mnajua kwamba sisemi hili, kusema, "Mnaona! Niliwaambia!" Si—simaanishi hilo.

27 Natumai sitafikia mahali ambapo nitajifanya mwenyewe, mbele za watu, kuwa mjua yote. Ikiwa kamwe nitakuwa hivyo, tafadhali mtu fulani aje anisahihishe, na kuninyosha, na kusema, "Hapa, ngoja kidogo." Unaona? Sitaki kuwa hivyo.

28 Lakini Mungu akisema lolote, na inathibitika kuwa Kweli, na—nataka hilo lijulikane. Kwa sababu, si mimi niliyelisema. Ni Yeye aliyelisema. Sasa, nilikuwa . . .

29 Na kama nilivyosema Jumapili iliyopita, ninaamini ilikuwa, hapa. Nimekuwa katika mimbara hii miaka ishirini na minane, na hakuna wakati mmoja ambapo niliwahi kutaja siasa, kwa vyovyote hata kidogo, mpaka Jumapili iliyopita. Na niliwaambieni enyi watu kuomba tu kabla hamjaenda kwenye uchaguzi na kupiga kura.

30 Nilienda huko chini kwa Ndugu Wright, hivi majuzi, nami nadhani yeye ni mmoja wa walio na umri mkubwa kuliko wote, yeye na Ndugu Roy Slaughter, na wachache wa wale ambao wamenijua miaka hii yote. Wala Ndugu Wright hakujua jinsi nilivyopiga kura. Kamwe hakujua kama nilikuwa Mwanademokrasia au Mrepablikani. Na hayo ndiyo makazi yangu ya pili. [Ndugu Wright anasema, "Tumesafiri pamoja, tumeomba pamoja, kila mahali, na hujawahi kuniuliza kuhusu kura yangu, wala nami kukuuliza wewe."—Mh.] Haina maana kabisa, hiyo ndiyo sababu, Ndugu Wright. [Mtu mwingine anasema, "Ndugu Bill, ningesema jambo lilo hilo."] Asante. Asante. Mimi kamwe . . . Hakuna aliyejua jinsi nilivyopiga kura. Kwa sababu, vyama vyote viwili, hakuna kimoja kiwezacho kujivuna.

31 Lakini, juma lililopita, sababu nilikuwa nikitaja jinsi nilivyofanya, kulikuwa na zaidi ya siasa iliyohusishwa.

32 Ningetaka kuwasomeeni unabii uliotolewa. Nilianza . . . Na huenda . . . Jambo jingine, Bw. Mercier na wengi wa hao wanaenda kuchukua baadhi ya unabii huu wa kale, na kuuchunguza, na kuurudia kidogo, ama kuuleta kwa majira haya, na kuuweka magazetini. Ningependa kusoma mambo fulani ambayo ningewatakeni ku—ku . . . Hili, kwanza. Ningetaka kuwasomeni jambo fulani.

33 "1932." Sikilizeni hili. "Nilipokuwa njiani, ama nilipokuwa ninajiandaa kushika njia kwenda kanisani asubuhi ya leo, ilitokea kwamba niliingia katika ono. Ibada zetu zinafanywa katika Barabara kuu ya Meigs, kwenye maskini makazi ya yatima ambapo Charlie Kern anaishi katika sehemu moja ya hilo jengo." Yeye anaishi upande wa pili tu wa barabara sasa, mwajua. "Basi ikawa, ya kwamba, nilipokuwa katika hili ono, niliona mambo fulani ya kuogofya yakitendeka. Ninasema hili katika Jina la Bwana.

34 "Rais aliye mamlakani sasa, Rais Franklin D. Roosevelt," sasa kumbukeni, hii ni miaka ishirini na minane iliyopita, "atasababisha ulimwengu wote kuingia vitani. Na mtawala mpya wa kimabavu wa Italia, Mussolini, atafanya uvamizi wake wa kwanza kuelekea Ethiopia. Na atanyakua Ethiopia, lakini hiyo itakuwa yake ya mwisho. Atafikia mwisho wake.

35 "Tutakuwa katika vita na Ujerumani. Angalieni Urusi. Sasa, hilo, unaona, Ukomunisti, Unazi, na Ufashisti. Angalieni Urusi, bali hiyo siyo hasa ya kuangalia.

36 "Itakuwa pia . . . kumekuwa na uovu uliofanywa katika nchi hii, wameruhusu wanawake kupiga kura. Hili ni taifa la mwanamke, naye atalichafua taifa hili kama Hawa alivyochafua Edeni." Sasa mnaona ni kwa nini ninakemea jinsi ninavyokemea? Nina BWANA ASEMA HIVI. "Katika kupiga kwake kura mwanamke, atamchagua mtu asiyefaa.

37 "Wamarekani watapata pigo kubwa mahali ambapo Ujerumani itajenga, ambao utakuwa ni ukuta mkuu wa saruji," Ngome ya Maginot, miaka kumi na moja kabla haijajengwa, "lakini hatimaye watakuwa washindi.

38 "Basi wakati wanawake hawa wanaposaidia kumchagua mtu asiyefaa, ndipo niliona mwanamke mashuhuri akiinuka Marekani, amevalia nadhifu na ni mrembo, ila ni katili moyoni. Ama ataelekeza au kulipeleka taifa hili katika uharibifu." Ninayo, katika mabano, "(Labda, kanisa Katoliki).

39 "Pia, sayansi itaendelea, hasa katika ulimwengu wa mitambo. Magari yatazidi kuchukua umbo la yai. Hatimaye wataunda moja ambalo halitahitaji usukani." Wanalo sasa. "Litadhibitiwa na nguvu fulani.

40 "Kisha nikaona Marekani kama panapoungua, mahali palipoteketezwa kwa moto. Mwisho utakuwa umekaribia." Halafu ninayo, katika mabano, "(ninabashiri kwamba hili litatendeka . . .)." Sasa, kumbukeni, Bwana, hilo ndilo Bwana aliloonyesha. "(Bali nabashiri hili litatendeka kabla ya 1977.) Juu ya ubashiri huu, ninaweka msingi, kwa sababu ya maangamizi ya haraka yanayokuja sasa, jinsi yalivyokuwa yanasonga upesi, muda ule utakaopita kabla ya taifa hili kufikia mahali pake."

Sasa, angalieni kilichotukia sasa.

41 Ambapo Rais Franklin D. Roosevelt, alipeleka Marekani kwenye karamu ya chai ya Uingereza. Hiyo ni kweli. Ujerumani haikutuonea kamwe; sisi ndio tuliwaonea. Ikatupa ulimwengu mzima vitani, iliyosababisha vita vya dunia. Ujerumani ilijenga Ngome ya Maginot. Ambayo, hapo, mtu yeyote wa kale hapa anajua kile ilichopeleka pale kwenye Ngome ya Maginot.

42 Wanawake, walipopewa haki ya kupiga kura, walimchagua Rais mteule Kennedy, ilikuwa ni kura ya wanawake, mtu asiyestahili; ambayo hatimaye itaelekeza kwenye utawala mkamilifu, wa kanisa Katoliki, katika Marekani. Halafu bomu linakuja linalomlipua.

43 Yapo mambo saba yaliyobashiriwa, na matano kati ya hayo yametukia tayari. Kwa hiyo unaweza kujiamulia, mwenyewe, kwamba tuko mbali kiasi gani. Tumekaribia mwisho. Kama

mambo hayo matano yametukia, haya mengine mawili hayana budi kutukia. Hayana budi tu kutukia.

44 Sidhanii kwamba Bw. Kennedy atakuwa na athari nyingi sasa, kwa sababu atakuwa Rais wa ajabu, ili kuwaingiza wengine, kuandaa mandhari kama tu waliyo nayo huko Uingereza, kama walivyofanya huko Mexico, kama walivyofanya kila mahali pengine namna hiyo. Na watu wa Marekani, vigeugeu sana; si kiroho. Ni werevu, ila ni werevu kupita kiasi kwa wema wao wenyewe. Akili hurudi nyuma, wakati mwingine, na kuenda kinyume na matarajio. Kwa hiyo wao . . . Ninahubiri juu ya hilo, asubuhi ya leo, baada ya kitambo kidogo.

45 Kwa hiyo, tunakuta, tuko—tuko ukingoni kabisa. Sababu ya mimi kusema hili; hiyo ndiyo sababu nilikaza hilo, hivi majuzi, kwa nguvu sana jinsi nilivyofanya. Lakini ilikuwa ni hiyo iliyofanya hivyo, hiyo ni kweli, kura ya wanawake. Hiyo iliweka . . .

46 Hivi mliona hiyo mikutano kwenye televisheni? Nixon kuwa karibu, karibu sana, na wanaume wote. Wote walitaka kumbusu Kennedy, wanawake, wakiruka kutagaa magari, kila kitu namna hiyo, wakirukaruka.

47 Na sasa hebu nilete kitu kingine. Sijaandika hapa, bali, kwenye kanda ya sumaku. Na hii inarekodiwa, pia. 1956, huko Chicago, Illinois, nikiwa nimesimama kwenye . . . ile shu- . . . Shule ya Sekondari ya Juu ya Lane Tech. Walikuwapo. Nikasema, "Mwaka huu utakuwa ni wakati wa mabadiliko kwa Marekani." Ndio kwanza nitoke ng'ambo, sijui ni kwa nini nimekuja. Nimerudi, nikafutilia mbali mikutano yangu huko Afrika na kote, nikarudi. Billy Graham, jambo fulani la ajabu, yeye alifutilia mbali yake. Tommy Osborn akafutilia mbali yake. Na sisi sote, tukivuka Marekani, katika mikutano. Nikasema, "Marekani ama itampokea au kumkataa Kristo, mwaka huu."

48 Ndipo nikasema, walipochagua, kule Indiana, mvulana mwenye umri wa miaka ishirini na miwili . . . mvulana mwenye umri wa miaka, kuwa hakimu. Roho wa Bwana alishuka juu yangu, na kusema, "Hatimaye watakuwa na Rais ambaye ni aina ya Rais anayenyoa kiduku, mpenda starehe, mpinga maadili, mtu anayependwa na wanawake."

49 Sasa, huo ni ubashiri, miaka iliyopita. Mnaona mahali tulipo? Muda umeenda kuliko tunavyodhania.

50 Hivyo basi, nafikiri kwamba Jumbe hizi juu ya hizi Nyakati Saba za Kanisa ziko kwenye wakati unaofaa. Hebu tuwe katika maombi, na kuchunguza.

51 Sasa, ukikosa kukubaliana na kusema, "Nafikiri Ndugu Branham amekosea." Hiyo, una haki kufanya hivyo. Lakini, kabla hatujafanya hivyo, kabla hujafanya, hebu tuchunguze yale Bwana aliyosema, kwa Maandiko. Tuone ikiwa . . .

52 Ndipo basi unabii, yale yaliyotolewa, kwamba yangetimia, kisha uangalie na kuona mahali yalipotimia, au la. Sasa, yako kwenye kanda na kadhalika. Mnajua nilinena, miaka kadhaa iliyopita, nayo haya hapa yanatimia sasa.

53 Mussolini alienda huko chini Ethiopia, sivyo? Maskini hao watu weusi huko chini wakiwa na—wakiwa na vifyekeo, panga, na fimbo, kupigana navyo. Na yeye, akiwa na mitambo ya kisasa, aliwaua tu kabisa. Akarudi, akijisifu juu yake, bali alipata maangamizi yake. Hiyo ni kweli.

54 Nao Wamarekani . . . Nao Wajerumani walijenga Ngome ya Maginot. Na wao . . . Ndipo Wamarekani wakapigwa vikali huko, bali hatimaye walishinda. Kweli kabisa. Nyinyi watu wa zamani, ndugu, mnajua hilo, nanyi nyote kwenye Siku Yenyewe, na kadhalika, na wakati walipoingia.

55 Sasa, na mnakuta basi kwamba wanawake, wamepewa haki za kupiga kura, nao wakamchagua Rais ambaye hawakupaswa kumchagua. Mnaona? Hilo ndilo lile anguko.

56 Na licha ya hayo, sasa, tunakaribia mkutano huu mwingine unaokuja. Basi iweni wenye kuomba, na muombe kwa bidii sasa, kwamba Mungu atatubariki na atafungua fahamu zetu, ili tupate kujua saa tunayoishi.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

57 Bwana wetu wa neema, kwa vile kwa njia moja, ni—ninajihisi nikitetemeka, kujua ya kwamba ulimwengu huu uko kwenye wakati wa mwisho. Nisingejua nikimbilie taifa gani. Hakuna kimbilio tena, ni kuangalia juu pekee. Kwa kuwa tunaambiwa, "Mambo haya yatakapoanza kutimia, basi angalieni juu, kwani ukombozi wetu unakaribia."

58 Ee Mungu, ninauombea ulimwengu wenye dhambi leo, katika hali yake, kuona jinsi kila kitu kinavyoendelea. Ninaomba ya kwamba, kwa njia moja ama nyingine, Bwana, kwamba Wewe utanena na kila moyo, kila mhudumu, ili aweze kuwa mwale unaowaka moto katika siku hizi za mwisho, kuita kwenye toba, na kurudi tena kwa Imani, Kanisa la Mungu aishiye. Kama tujuavyo, tunaishi katika Wakati huo wa Kanisa la Laodikia, ambapo kwamba watakuwa vuguvugu. Ninaomba, Baba, kwamba Wewe utatujalia tushike sana kile tulicho nacho, Kristo, tukitazamia Siku ile ya kuonekana Kwake. Tusamehe dhambi zetu, kama tulivyowasamehe wale waliotukosea.

59 Basi tunajua sasa, Bwana, kwamba tunaona ulimwengu wa nje, tukijua kwamba ilibidi itimie. Hakuna njia ya kuikomesha. Japo tunanena dhidi yake, na kutoa sauti kuipinga, hata hivyo, tunajua mioyoni mwetu, kulingana na Neno Lako, itafanyika, kwa vyovyote vile, kwani Wewe umesema hivyo. Bali katika Siku hiyo ya Hukumu, wakati kanda kubwa ya Mungu ya sumaku itakapochezwa, tunataka sauti yetu kupinga makosa na kutetea haki.

60 Tutie moyo leo hii, Bwana, kwa Uwepo Wako. Wabariki wahudumu hawa wote waliopo hapa, na walei wote wa kanisa. Wote waliozaliwa upya kote ulimwenguni, vijinga vikuu vya moto ambavyo Wewe unavyo kwenye redio, na huko nje katika sehemu zingine za ulimwengu, wakihubiri Injili; wamishenari wakishinda njaa, waume na wake chini ya mateso makuu, wangali wamesimama kwenye wajibu wao. Mungu, wabariki leo.

61 Na katika maskani hii ndogo, tupe baraka Zako, Bwana. Tutie upako. Wabariki wale walioimba, asubuhi ya leo, nyimbo za ajabu za Sayuni, tulizozifurahia moyoni mwetu, kote katika miaka, tukijua kwamba siku moja tutasimama na kuimba nyimbo hizo katika Uwepo wa Mwana-kondoo. Libariki Neno, leo hii, uutie Ujumbe upako, Bwana. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

62 Ninataka kuvuta usikivu wenu, asubuhi ya leo, kwenye Maandiko yanayopatikana katika Kitabu cha Mwanzo. Na sasa nitajaribu kupitia moja kwa moja upesi, juu ya Ujumbe huu, Bwana akipenda, kwa sababu tunataka kuwaombea wagonjwa na kuwa na ibada ya ubatizo. Ninataka mfungue Kitabu cha kwanza cha Biblia, mlango wa kwanza wa Kitabu. Mwanzo, mlango wa kwanza, na hebu tuanze kusoma kutoka kifungu cha 9.

> *Mungu akasema, maji yaliyo chini ya* mbingu *na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane; ikawa hivyo.*
>
> *Mungu akapaita pale pakavu Nchi; na* akakusanya *makusanyiko ya maji akayaita Bahari; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.*
>
> *Mungu akasema, Nchi na itoe majani,* na mche *utoao mbegu, na . . .* miti *ya matunda izaayo matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo.*
>
> *Nchi ikatoa majani, na* miche *itoayo mbegu kwa jinsi yake, na* miti ilizaa *matunda, ambao mbegu zake zimo ndani yake, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.*

63 Sasa ninataka kuchukua kifungu juu ya somo la: *Hukumu Kwa Uwakilishi.* Na hebu Bwana aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake.

64 Majuma mawili au matatu yaliyopita nilikuwa nikipitia kwenye majimbo ya magharibi. Na nilikuwa nikiangalia kote, nikiendesha motokaa mwenyewe, nikienda kukutana na Wafanyabiashara Wakristo huko Idaho. Nami nilishangazwa nilipotazama vibao, matangazo. Karibu unaweza kutazama kote na kuona kilicho akilini mwa watu na kilichoko mioyoni mwao.

65 Kama ambavyo nimesema mara nyingi, hebu niende katika nyumba ya mtu, na hebu tuone aina ya muziki wanaosikiliza. Hebu nione aina ya vitabu wanavyosoma, na aina za nyimbo wanazoimba, aina ya picha walizo nazo nyumbani mwao. Karibu ninaweza tu kukwambia kilicho tabia ya mtu huyo. Unaona? Ni kwa sababu, wao, haijalishi wanachoshuhudia, vinginevyo, matunda yanathibitisha kile kilicho.

66 Pia nilitambua kwamba sisi ni taifa kuu la kisayansi, ulimwengu wa kisayansi. Tena niliona kwenye vibao vya matangazo, hasa katika ukanda wa mahindi wa magharibi, na kadhalika, ilikuwa ni picha ya mwanamume aliyeshika suke la mahindi, akipukusa mahindi, akisema, "Jamani, jinsi haya yalivyo mahindi mazuri!" Nayo yalikuwa ma—mahindi maarufu chotara. Basi kwa njia fulani, huku nikiwazia juu ya hilo, nikisafiri, peke yangu . . .

67 Wala huwezi kuifungua redio yako tena, kwa sababu, hasa katika maeneo ambayo kila kituo ni maskini muziki huu wa bugibugi na upuuzi huo wote, unajua, roki. Nawe kabisa huna . . . isipokuwa, ikitokea tu kwamba uifungue tu kwenye saa hiyo, na kupata habari na hali ya anga, halafu inakubidi kuizima tena.

68 Hivyo basi ninaamini, labda, Bwana alikuwa ananisaidia. Ndipo nikaandika nyuma ya ramani yangu ya barabara, "chotara," kwa sababu kitu fulani kilinigusa nilipoyaangalia, punje kubwa nzuri mno, za mahindi. Nikawazia, "Hayo ni tofauti sana na mahindi tuliyokuwa tukipanda." Kila kitu kinakuwa chotara. Lakini hivi ulijua ya kwamba hakifai kitu? Hakina uhai ndani yake. Hakiwezi kujizaa tena. Huwezi kupanda mahindi chotara. Ukipanda, u—una maskini shamba lililodumaa tu, kwa sababu ni chotara.

69 Ndipo nikapanda juu mlimani. Na—naye mmoja wa viongozi aliyekuwa pamoja nami, alikuwa ni m—mfugaji kuku. Naye, akifuga kuku, basi aliongoza tu juu milimani kwa ajili ya burudani. Mtu mzuri sana! Na wakati alipogundua kwamba mimi ni mhubiri, mbona, upesi alianza kunizungumzia kuhusu kuku chotara. Basi, alipofanya hivyo, hilo lilirejesha fungu langu dogo nililoandika kwenye ramani yangu ya barabara, "chotara."

70 Vema, tukiwa tumejilaza kwenye mikoba yetu ya kambi kwenye theluji, juu mlimani, nikamwambia, "Ningependa kujua zaidi kuhusu kuku wa aina hiyo."

71 "Vema," akasema, "sayansi kweli imefanya jambo kuu." Kasema, "Wamezalisha kuku na vitu mbalimbali, hata wamefikia mahali ambapo karibu kuku hawana miguu, ama kuku hawana mabawa. Yote ni kidari tu." Ila akasema, "Sehemu mbaya inakuja sasa, kwamba watu hawamtaki, kwa sababu ni nyama laini sana. Naye kuku huyo huishi mwaka mmoja tu, na anakufa."

72 Karibu amekufa, kwa kuanzia. Unaona, ni kuchanganya mbegu. Si sahihi; hakufai. Na wengi wa watu sasa wanaotaka kuwa na chakula kitamu cha jioni cha kuku, huenda huko mashambani na kujinunulia kuku aliye na miguu, anaweza kuchakura, na mabawa, anaweza kuruka. Naye ni—ni—ni kuku, jinsi Mungu alivyomwumba. Bali ni kuchotarisha kuku kumemfanya kuwa kidari tu, naye hutembea akianguka-anguka. Na inawabidi kumweka kwenye kiwambo. Hawawezi kumweka nje; hawezi kuchakura. Hawezi kujitafutia chakula. Nayo nyama imekuwa, mbaya sana, hata hawawezi kuitumia. Na iwapo kuku huyo amefanywa kuku wa kutaga, mayai yake hayataanguliwa. Na halafu, jambo jingine, kuku huyo hutaga mayai hata kufa, katika mwaka mmoja. Anaishi mwaka mmoja tu. Ndipo nikawaza, "Vema, sasa, huyo ni kuku kweli!" Kuchanganya mbegu, kuharibu kile Mungu alichoumba.

73 Halafu tulikuwa na mlolongo wa nyumbu tuliobebea mizigo. Nami ninatambua ya kwamba nyumbu ni chotara, pia. Kamwe usimlaumu Mungu, kwa kumwumba nyumbu. Mungu kamwe hakuhusika katika hilo. La. Huyo alikuwa ni mwanadamu. Nyumbu hajui yeye ni wa wapi. Ha—hawezi kujizaa tena. Yeye ni—yeye ni chotara. Mnaona? Ha—hajui baba yake ni nani, wala aliyekuwa mama yake. Naye hawezi kuzaa tena. Yeye ni nyumbu tu, naye yuko kwenye njia itelezayo, ya kuelekea mautini. Basi haijalishi ni kiasi gani anajaribu kuzaa wa aina yake, hawezi. Hayo yote ni kinyume na Neno la Mungu.

74 Mungu alisema hapa, katika Mwanzo 1:11, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake, kwani uhai uko ndani yake. Kila mbegu na izae kwa jinsi yake."

75 Lakini mwanadamu anajaribu kuonyesha ya kwamba yeye ni mwerevu kuliko Muumba wake. Anataka kuthibitisha ya kwamba anajua zaidi kuhusu jambo hili kuliko Mungu anavyojua. Kwa hiyo, basi, yeye daima, kupitia sayansi, anajaribu kumwonyesha Mungu kwamba anajua mengi juu yake kuliko Yeye anavyojua. Naye Mungu humwacha aendelee, kupitia kwa utafiti wake wa kisayansi. Na, katika kufanya hivyo, yeye hujiua mwenyewe. Mungu huacha ujinga wake mwenyewe umwue.

76 Mama yangu, huko nyuma, alizoea kusema, "Mpe ng'ombe kamba ya kutosha, hujinyonga mwenyewe." Vema, hiyo ni kweli. Nawe unaacha tu. . . Mungu alimwacha tu mwanadamu aende ajinyonge kwa ujinga wake mwenyewe. Kamwe hatakuwa mwerevu kuliko Mungu. Mungu anajua kilicho sahihi. Lakini, wanadamu, kupitia kwa kuchanganya mbegu, wanajaribu kuzalisha bidhaa bora kuliko kile alichoumba Mungu.

77 Sasa, Mungu, wakati alipoliumba Kanisa Lake, aliumba Kanisa la kipentekoste. Hilo lilikuwa la asili, Kanisa la

kipentekoste lililojazwa na Roho Mtakatifu, wanaume na wanawake wanaoongozwa na Roho wa Mungu.

78 Wanadamu hawangeweza kuacha hilo peke yake. Alitaka kuchotarisha kanisa. Kwa hiyo akazalisha ndani, ulimwengu, pamoja nalo: theolojia, mafundisho, madhehebu. Loo, hakika, inafanya kanisa maridadi zaidi. Jamani, naam! Jinsi lilivyo tofauti na Kanisa asili. Loo, tunayo majengo makubwa, wahubiri wenye elimu, tabaka bora la watu, waliostawi, waliovalia bora zaidi; wakiweka majina yao ndani yake, na pesa zao ndani yake, kulistawisha; wakiwatuma wahudumu wao kwenye seminari, kupiga msasa elimu yao na theolojia. Wakati wote, wakiwapeleka mbali zaidi na Mungu.

79 Hilo halikuwa ni mpango wa Mungu, kwa kuanzia. Kamwe hakumtuma mmoja wao kwenye seminari yoyote. Yeye aliwatuma kwenye chumba cha juu, kungoja huko mpaka Roho Mtakatifu alipokuja juu yao, ili wawe wahudumu wa Bwana waliowekwa wakfu.

80 Bali, kuchanganya mbegu, kulileta kanisa kwenye theolojia, badala ya kumwacha Roho Mtakatifu aliongoze. Waliingiza maaskofu, waangalizi wakuu. Wakati, Roho Mtakatifu ndiye Kiongozi asilia wa Mungu wa Kanisa. Lakini wanachotarisha kanisa, kama walivyofanya kuku, kama walivyomfanya nyumbu, kama walivyofanya kila kitu kingine. Kuchotarisha, kulifanya tofauti. Kuingiza ndani ulimwengu, mambo ya ulimwengu; michezo ya basketboli, na milo ya supu ya jioni, na—na michezo ya karata, na namna zote za mambo ya ulimwengu. Ni kweli, ni maridadi zaidi. Ni jengo kubwa zaidi, tabaka la watu waliostaarabika. Uimbaji wao huenda ukawa wenye utaratibu zaidi katika sauti, na kadhalika, kuliko m—mpentekoste wa mtindo wa kale akiwa na tari na gita. Ila hauna Mbegu. Hauna sauti ya kusikika kwao. Wanauelezea vinginevyo, Wote, "*Huu* ni bora kuliko Ule ulivyokuwa."

81 Kama wanavyojaribu na mahindi chotara, "Ni bora kuliko ya kale yalivyokuwa." Hayakuwa bora. Uhai ndani yake haukuwa bora. Upande wa nje huenda ulionekana bora, bali uhai haukuwa sahihi.

82 Nasi tunazungumza kuhusu uhai. Uhai si sahihi, katika kuchotarisha. Mungu anautaka jinsi alivyoufanya hapo mwanzo.

83 Hivyo basi, kanisa limekuwa chotara. Na sasa inafikia mahali ambapo kanisa zaidi sana ni kama chama, kuliko lilivyo kama baraka ya kipentekoste. Wasomi ni waelimishaji zaidi kuliko walivyo wahubiri. Zaidi sana wao ni mahali pa—pa kupata elimu kubwa. "Mchungaji wetu ana Digrii ya Uzamifu," ama—ama kitu kama hicho, "ya theolojia."

84 Wala hawawezi kujizalisha tena. Maridadi kama ilivyo, hawawezi kujirudia wenyewe. Ungewezaje? Hawawezi

kujizalisha wenyewe. Jaribu kuzalisha Methodisti na Baptisti uone kile ulicho nacho. Una haini mbaya zaidi kuliko uliye naye hapo mwanzo. Hiyo ni kweli. Huwezi. Una kibushuti. Hiyo ni kweli.

85 Ukipanda mahindi chotara, yanakua karibu namna *hiyo* na kugeuka manjano. Hakuna uhai ndani yake. Hiyo ndiyo sababu hayawezi kuzaa.

86 Na hiyo ndiyo shida na kanisa siku hizi. Halina Uzima ndani yake. Lina maonyesho chungu nzima, na ta—tabaka bora la watu, wanavyojiita. Punje kubwa zaidi, majengo maridadi zaidi, wahubiri walioelimika zaidi, bali hakuna Uzima humo ndani wa kuzaa tena watoto waliozaliwa upya. Haliwezi kujizaa tena. Wakati, Punje ilipandwa kwanza. Pili, wakaingia, kisha wakaichotarisha. Na muda si muda wajua, haiwezi kurudi. Ninamwomba msomi yeyote kuenda nami kwenye historia. Kanisa lolote lililowahi kuacha msingi wake wa asili, halijawahi kuinuka tena.

87 Wakati Mungu alipomtuma Luther naye akawa na uamsho, alifagia ulimwengu. Ila aliliundia dhehebu, na kulichanganya na ulimwengu, kama kanisa Katoliki. Na wakati alipolichanganya, alifanya nini? Alizalisha kundi la mahaini, chotara. Na hajainuka kamwe wala hatawahi kuinuka.

88 Baadaye akaja John Wesley na kufanya jambo lile lile, na uamsho. Punde tu yeye na—na Asbury na waanzilishi wa kale walipokufa, waliliundia dhehebu na kutengeneza kanisa la Methodisti ya Kiwesley. Na kamwe hawajainuka, wala hawatainuka, tena.

89 Kanisa la Anglikana, kitu kile kile, kutoka kwa Calvin. Walipokuwa na uamsho, lilikuwa sawa. Ndugu Simpson, pakiti mfukoni mwake sasa, kutoka Canada. Kanisa la Anglikana, sasa wameingia, wahudumu na hao wote, katika ulevi. Wanachanganya bia yao, na pombe kali na kadhalika, pamoja, moja kwa moja kanisani, kuwa na karamu, na kunywa pombe. Ni kitu gani? Haliwezi kurudi kwenye asili yake tena, kwa sababu limechanganywa na ulimwengu. Limepotea.

90 Sasa, tunazungumza kuhusu Anglikana, na Methodisti na Baptisti, lakini Pentekoste ni vile vile. Miaka michache iliyopita, tulikuwa na Kanisa la kipentekoste lililokuwa linawaka moto. Lakini walifanya nini? Walilichotarisha, wakaliundia dhehebu, wakalirudisha ulimwenguni. Sasa mna nini? Hasa tu kama vile Mungu alivyofanya na nyumbu. Liko katika barabara yake itelezayo ya ibilisi. Kamwe halitarudi. Limekwisha, limejiundia dhehebu na kuanguka. Na sasa wana makanisa mazuri zaidi. Loo, watu wa kipentekoste walizoea kuwa kwenye misheni ndogo pembeni mwa uchochoro, walikuwa wakipigwa teke, huku na huku, na kutupwa gerezani, nusu ya muda, kwa ajili ya kupaza sauti usiku kucha. Vema, hakika wangekuwa na wakati

mgumu kupata mmoja sasa. Kulifanyika nini? Walilizalisha kichotara. Walilifanya kama Baptisti; kama Baptisti ikifanywa kama Methodisti; Methodisti ikifanywa kama Luther; Luther akifanywa kama Katoliki. Umepata kitu gani? Kundi chotara la punda mwitu. Hiyo ni kweli.

91 Kitu kipumbavu kuliko vyote nikijuacho ni nyumbu. Hana hisia za kibinafsi hata kidogo. Atavuma karibu nawe mpaka saa ya mwisho ya kifo chake, apate kukuua. Hajui chochote ila "gii" na "hoo." Hana hisia ya moyoni. Hajui baba yake alikuwa ni nani, ni nani aliyekuwa mama yake, na mahali anakoelekea, ama mahali alikotoka.

92 Hiyo ni karibu kama watu wengi leo hii, karibu sawa tu. Hivi uliwahi kuona nyumbu? Unaweza kuzungumza naye, naye atasimama hapo huku ameinua masikio; angalia, uso huo mkubwa mrefu na hayo masikio yametokeza. Hivyo ndivyo wengi wa hawa punda wafanyavyo, hiyo ni kweli, wanasimama tu, wanakuangalia, wanalia, "Siku za miujiza zimepita. Huo uponyaji wa Kiungu, na kunena kwa lugha, na Roho Mtakatifu, hakuna kitu kama hicho." Hiyo ni kweli. Dini ya nyumbu! Hiyo ni kweli. Chotara! Hayo ndiyo yote ajuayo. Hawezi kujua chochote kingine. Achana naye. Hebu na tuendelee na Mungu. Chotara, nyumbu tu, hajui alikotoka. Hana ukoo safi. Hawezi kuwa wa ukoo safi.

93 Lakini farasi ni tofauti. Naam, bwana. Ukichukua farasi mzuri, wa ukoo safi, yeye ni mpole tu na mzuri. Anapenda kufika hapo na kurukaruka, wajua, kisha anarudi, anaweka kichwa chake juu ya mabega yako, na kulia na kuendelea. Yeye ni—yeye ni mnyama mzuri. Ni mwaminifu; anasimama na wewe. Kwa nini? Anajua. Anayo makaratasi kuonyesha ya kwamba yeye ni wa ukoo safi. Amina. Imeandikwa, kwamba yeye ni wa ukoo safi. Damu yake ni safi.

94 Hivyo ndivyo ilivyo na mtakatifu wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili. Unaweza kumwambia, "Yesu Kristo ni yeye yule jana na milele." Anapaza sauti, "Amina." Kwa nini? Yeye ni wa ukoo safi. Ujuzi wake umeandikwa katika Biblia. Amezaliwa kwa Damu ya Yesu Kristo, naye ni Mkristo ukoo safi. Utukufu! Hakuna kuchanganya mbegu hapo. Yeye ni halisi, mpole, mnyenyekevu. Unaweza kumfundisha kitu.

95 Hujaribu kutii. Unaweza kumpeleka nje kwenye maonyesho, karibu umfanye kuwa kama mwa—mwanadamu. Atainama, alie, aruke. Hujawahi kumwona nyumbu akifanya hivyo. Huwaoni nyumbu katika maonyesho yoyote, wakitenda namna hiyo, maana hawana sifa hiyo, kwa kuanzia.

96 Hiyo ndiyo sababu Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anaweza kukubali uponyaji wa Kiungu. Mkristo aliyezaliwa mara ya pili anaweza kumkubali Roho Mtakatifu, kwa sababu kuna Kitu fulani ndani yake, Kitu fulani ndani yake, kumfanya aamini.

Roho wa Mungu mle ndani, akilihakikisha Neno la Mungu, kwamba yeye ni ukoo safi. Naam.

97 Lakini nyumbu hawafanyi hivyo. Hawawezi. Hakuna kitu ndani yao kuwafanya wafanye hivyo nacho.

98 Sasa, juu ya huku kuchotarisha. Mnajua, Hawa alikuwa ndiye mama wa kuchotarisha. Alichanganya vibaya jamii ya wanadamu, mwajua, baada ya yeye kufanya jambo hili ovu. Nami ninajua hii iko kwenye kanda, kwa hiyo tutaifanya mtindo wa kitoto kwa ajili yao, wakitaka. Lakini wakati alipofanya tendo hili na yule nyoka; ambaye hakuwa nyoka, ama reptilia. Biblia ilisema, "Alikuwa ndiye mwerevu kuliko hayawani wote wa kondeni."

99 Sayansi inajaribu kutafuta sasa, wao, mifupa ya kiumbe fulani kati ya tumbili na mwanadamu, na kuiweka kwa watu weusi, na kadhalika namna hiyo. Wao ni wajinga kama wawezavyo kuja.

100 Nyoka alikuwa ni mtu. Damu ya mnyama haitachanganyikana na damu ya mwanadamu. La, bwana. Lakini spishi hii ilikuwa karibu sana, hapo katikati, mpaka akachanganyikana, na Shetani alijua hilo. Jamaa mkubwa mno! Si ni ajabu kwamba walipata majitu wakubwa nchini baada ya hili? Laiti Josephus, yule mwandishi, angefikiria hilo. Hao majitu walitoka wapi? Uzao wa nyoka. Biblia ilisema ya kwamba ange—angefanya uzao wa nyoka . . . "Uzao wa nyoka," nyoka alikuwa na uzao, "na uzao wa mwanamke." Lakini afadhali tuachane nao. Hawaamini hilo, kwa hiyo tunawachukua tu katika hali yao ya utoto. Lakini wakati alipofanya hivyo, alichafua kitu chote.

101 Sasa usikifikishe kwenye kitu hicho cha aibu, tafadhali, cha mtofaa. Kama ambavyo nimesema mara nyingi: ikiwa kula matofaa kuliwafanya wanawake kutambua kwamba walikuwa uchi, heri wapitishe matofaa tena, maana wa—wakati umewadia. Sisemi hilo kuwa fidhuli. Bali ninalisema, ku—kutoa hoja, kwamba ni kweli. Haikufaa matofaa. Hebu tusiwe wa dhihaka hivyo kulihusu. Haukuwa ni mtofaa.

102 Lakini hebu tuliweke kwenye mti mwingine, kusudi tuweze kulileta na kutimiza somo letu. Hebu tuuchukue, mti wa imani, kwamba Hawa alikula mti huu uliokatazwa wa kutokuamini. Basi tunaweza kufanya somo hilo litokee. Ilikuwa ni imani. Hakuliamini Neno la Mungu. Mungu alisema jambo fulani-fulani litafanyika; alipaswa kuachana Nalo. Alipaswa kuliamini jinsi Mungu alivyolisema. Lakini, la, Shetani akaja na theolojia yake, naye akalichanganya, na kumpa Adamu, na ikasababisha imani chotara.

103 Hiyo ndiyo kanisa imepata leo hii, linalojiita kanisa, imani chotara. Imechanganywa na hofu, mashaka, mahangaiko. Kama ilikuwa ni Imani halisi, isingetikisika. Mungu anaposema lolote,

ingekuwa hivyo. Lakini, unaona, alilichanganya, akachukua yale Mungu aliyosema na yale Shetani aliyosema, akayasuka pamoja, na kusema, "Hili hapa."

104 Hivyo ndivyo watu wengi wafanyavyo leo hii. Mnaona, wanachukua kile Biblia isemacho na kile mwanadamu asemacho, wanafanya imani chotara. Basi wanapofanya hivyo, wanairudisha, "Loo, inafanya kanisa maridadi." Hakika. Bali hakuna Uzima ndani yake. Limekufa, imani chotara! "Loo, ninaamini ya kwamba Mungu alikuwako, naam, ila sasa Yeye si mponyaji leo." Hiyo ni imani chotara. "Ninaamini ya kwamba aliwapa wapentekoste Roho Mtakatifu huko nyuma kwenye Siku ya Pentekoste, bali hiyo si kwa ajili yetu leo." Imani chotara, iliyohukumiwa na Mungu. Chotara, haifai kitu! Kaa mbali nayo. Ni ovu. Huleta mashaka. "Labda nitaenda huko juu nikaponywe. Labda Bwana ataniponya." Hiyo ni imani chotara. Haifai kitu. Hiyo ni imani ya kanisa.

105 Tunataka Imani ya Mungu. Mungu alisema jambo fulani, na Hilo ni Kweli. Kaa Nalo. Amina. "Loo! Laiti maneno yangu yangaliandikwa kwa kalamu ya chuma." Dumu na yale Mungu aliyosema. Ni Kweli.

106 Imani chotara, itasoma Waebrania 13 na kusema, "'Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele,'" Waebrania. Ndipo basi imani chotara inaingia, "Vema, kwa njia fulani, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, lakini Yeye si . . . Hawezi kuponya, leo, maana huo uko nje ya mpango Wake."

107 Lakini Imani halisi itasema, "Yeye ni yule yule." Si chotara. Haija—haijatiwa tu ukanisa pamoja na theolojia ya binadamu; si dini ya nyumbu, neno la mwanadamu na Neno la Mungu yakichanganywa pamoja kama mzabibu uliopotoshwa.

108 Yesu alisema, "Haikuwa hivyo pale mwanzo." Na si hivyo kwenye mwanzo. Mungu alitaka kila mbegu izae kwa jinsi yake. Basi tukichotarisha chochote, tunaharibu mpango wa Mungu. Chukua ua, ua la asili, urujuani, ni samawati . . . ama jeupe. Achana nalo, litarudi kuwa jeupe. Inakubidi kuendelea kulizalisha, wakati wote. Mungu hufanya vitu tofauti. Anavipenda tofauti. Na kuchanganya mbegu ni kitu hatari sana na cha kuchukiza hata kinaharibu mpango wa Mungu. Huvuruga jamii ya wanadamu.

109 Mungu hata alisema, katika Kumbukumbu la Torati, kwamba, "M—mtoto haramu hata asingeruhusiwa kuingia katika kizazi . . . katika kusanyiko la Bwana, kwa vizazi kumi." Hivyo ndivyo uzinzi ulivyo mbaya. "Vizazi kumi," kumi mara arobaini, miaka mia nne. Kabla ya chotara . . . Mwanamke aliyeolewa na mwanamume, ama mwanamume aliyemwoa mwanamke, ambaye atavuka mipaka ya ndoa takatifu, na kuleta mtoto haramu, vizazi hivyo havitaingia katika Ufalme wa Bwana hadi vizazi kumi. Kumbukumbu la Torati 30 . . . 23:2.

Vema. Hataingia, mtoto haramu, yeye ama kizazi chake, ama kizazi chake, ama kizazi chake, hata ingawa wanajaribu, kama vile Esau, akilia apate mahali. Inachukua vizazi kumi. Miaka arobaini ni kizazi kimoja.

110 Mnaweza kuona ulimwengu huu wa kuchukiza, uliooza uko tayari kwa hukumu? Mwovu sana! Kuchanganya, kuchanganya kile Mungu ameunganisha; mwanamke kuishi kwa uchafu kwa mumewe; mume kuishi kwa uchafu kwa mkewe; na kuleta mtoto chotara. Loo, mwanamke fulani aseme, "Loo, si ana sura nzuri? Jamaa mkubwa, mnene, mrefu!" Hilo ni jambo lile lile, labda, Hawa aliwazia. Akamzaa mtoto haramu. Naye huyo mtoto haramu alikuwa ni Kaini, na kupitia Kaini wakaja majitu.

111 Daima imekuwa ni kitu kilicholaaniwa na Bwana. Chotara! Kaa mbali nacho, dini chotara. Usiichanganye.

112 Yesu alisema, "Ukiwa na imani ya mbegu ya haradali." Ni kwa nini Yeye, "Kama mbegu ya haradali"? Sukuma wiki na mchicha, zikichanganywa pamoja, huleta rapa. Bali haradali haitachanganyikana na chochote. Haradali, haradali halisi, huifanyi chotara. Ni haradali.

113 Watu waliozaliwa na Roho wa Mungu ni wana na binti za Mungu. Hawachangamani na ulimwengu. Wao si chotara. Wanadumu na Mungu. Wanadumu na mpango Wake. Wanadumu na Roho Wake. Hawataki chochote cha vitu chotara. Haileti . . .?. . . jinsi makanisa hayo mengine yanavyoonekana makubwa na yaliyopambwa, jinsi kusanyiko linavyoonekana kubwa na kupambwa, jinsi walivyo na mikutano mikubwa na ya kuvutia macho, hilo haliwasumbui hata kidogo. Daima niliupenda ule wimbo, "Nifundishe, Bwana, kungojea, huku mioyo inawaka moto," wakati wanapojenga majengo makubwa na kuwa na mambo makubwa.

> Nifundishe, Bwana, kungojea, huku mioyo inawaka moto,
> Jalia nidhalilishe kiburi changu, niliitie Jina Lako;
> Nifundishe nisitegemee yale wafanyayo wengine,
> Bali kungoja katika maombi nipate jibu kutoka Kwako.
>
> Kwani wale wamngojeao Bwana, watafanya upya nguvu zao,
> Watapaa juu, kama mabawa pamoja na tai,
> Watapiga mbio wala hawatachoka; wakitembea, hawatazimia;
> Ee, nifundishe, Bwana, nifundishe, Bwana, kungojea.

114 Usichukuliwe na mambo ya uchotara. Si sahihi. Hatimaye utafikia mwisho wake. Hauwezi kurudi. Wakati ni chotara,

kimekwisha. Hakiwezi kamwe kujizaa tena. Kikizaa, ni kibushuti.

115 Angalia kile . . . angalia kile, uamsho wa Wesley, tunapofikia Wakati huo wa Filadelfia, jinsi walivyokuwa na uamsho. Angalia uamsho unaofuta, angalia uamsho unaofuata, unaendelea tu kudumaa, kudumaa, kudumaa, kudumaa, mpaka sasa. Angalia mahali ulipo sasa. Angalia mahali Wabaptisti walipoanzia, wakiwa na John Smith, angalia mahali imedumaa kufikia. Waangalie Wapentekoste, walianzia mwaka wa 1906. Wakajichanganya na ulimwengu, wakaingiza mambo ya ulimwengu, na fundisho la ulimwengu. Walichukua, badala ya Roho Mtakatifu, kupeana mkono. Walichukua, badala ya kutumbukiza, kunyunyizia. Walichukua, kwa ubatizo wa maji, Jina la Yesu Kristo, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," kama ulimwengu. Walichukua kupeana mkono, kupokea Roho Mtakatifu, badala ya kunena kwa lugha na nguvu za Mungu kufuata. Waliweka uponyaji wa Kiungu katika ofisi ya daktari, badala ya magoti yako katika maombi. Walijichotarisha wenyewe. Nao wanadumaa, kila mwaka, wanadumaa. Mambo hayo hayako katika Biblia, hayo mafundisho. Bali ili kuwa maarufu, kujifanya wenyewe kanisa, kuyaunganisha jinsi yalivyo sasa, na muungano wa makanisa, kujiingiza ndani, ili kujifanya kama wale wengine, walifanya hivyo, na kujidumaza, wanaendelea kudumaa.

116 Kizazi cha kwanza cha wapentekoste walikuwa wanawaka moto. Kizazi cha pili kikaanza kufifia. Hiyo ni sasa. Angalia kile kizazi cha tatu kitakacholeta. Hakitatoka nje kabisa, kabla ya Yesu kuja. Kwa sababu, kanisa la Laodikia lilikuwa vuguvugu, si vuguvugu wala moto. Lingali lilikuwa na baraka kidogo iliyobaki ndani yake. Walichanganyika, mmoja *hapa*, na *pale*, na *kule* nyuma. Walichanganyika. Si baridi kabisa, bali vuguvugu. Mungu alisema, "Kanisa, katika msimamo wake, hata mnanichefua tumbo Langu. Wakati, nimewapa Roho Mtakatifu, nanyi mkamchanganya na ulimwengu, na kuruhusu mambo ya ulimwengu kuingia ndani. Nitalitapika tu shirika lote kutoka kinywani Mwangu."

117 "Lakini msiogope, enyi kundi dogo, Yule Ambaye amezishika Amri za Mungu. Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme." Dumuni na Neno. Kile Neno lisemacho, dumuni na Hicho. Msichanganye Hicho na chochote. Sijali ni askofu yupi, ni askofu mkuu yupi, ni mtu yupi anayesema chochote juu yake. Dumuni moja kwa moja na Neno.

118 Kama Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo." Kila mahali pengine katika Biblia, walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

119 Kamwe msikubali "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu" kwa ajili ya hilo. Mkikubali, mnajifanya wenyewe chotara. Sasa,

nionyesheni mahali pamoja katika Biblia ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa, "jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Hakuna. Ni theolojia iliyobuniwa na wanadamu ambayo imeingizwa ndani ya kanisa, ikapewa nafasi kuwa sanamu kama inayokuja kwenye taifa hili sasa.

120 Ninaweza kuwathibitishia, kwa historia na kwa Biblia, kwamba yeyote aliyebatizwa, "jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," amebatizwa katika kanisa Katoliki. Kwa ketekismo yao wenyewe, walisema, "Je, yeyote wa Protestanti ataokoka?" Kasema, "Baadhi yao. Wanakubali baadhi ya mafundisho yetu. Wanadai kuamini Biblia." Kasema, "Biblia ilisema, 'Tubuni mkabatizwe,' Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, na kadhalika, 'katika Jina la Yesu Kristo.' Biblia yao inafundisha hivyo. Bali wanakubali fundisho letu, hilo ni 'Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.'" Hiyo ni—hiyo ni katekismo.

121 Si fundisho la Kiprotestanti. Ni fundisho la Kikatoliki. Bali sisi, kama Wapentekoste, tulilichanganya na theolojia ya kujibunia. Mnaona mahali tunapoelekea? Si ajabu Mungu hawezi kutuma uamsho; hana kitu cha kuujenga juu yake.

122 Basi, atachukua watu binafsi, na kuujenga juu ya hao watu binafsi, na kuwatangaza mbele za ulimwengu, wale wanaodumu na hilo Neno.

123 Kunyunyizia, ni nani aliyewahi kusikia kuhusu hilo? Kukubali ubatizo wa maji, kwa kutumbukiza; uondolee mbali kutoka hapo, na kuufanya kunyunyizia. Ni nani aliyewahi kusikia kuhusu kuwapa mkono wa kuume wa ushirika, kuwaingiza kanisani, ama kwa barua? Upuuzi! Ni chotara.

Sote hatuna budi kupitia njia ile ile.

124 Mtu fulani alisema, "Mimi ni Mmethodisti kwa sababu mama yangu ni Mmethodisti." Mama huenda alikuwa Mmethodisti Mkristo, bali hilo halikufanyi mmoja. Huenda alikuwa ni Mbaptisti Mkristo, bali hilo halikufanyi mmoja.

125 Kama vile nimemnukuu David akisema, David duPlessis, akisema kwamba, "Mungu hana wajukuu." Mungu hana wajukuu. Mungu si babu. Hakuna mahali katika Biblia, paliposema Mungu ni "babu." Basi ni kwa nini mna wazo hilo la utatu lililovuka mipaka, "Mungu Baba, mmoja; Mungu Mwana, mwingine; Baba, na halafu Mungu Roho Mtakatifu"? Hilo linamfanya Mungu babu. Mungu hana wajukuu. Mungu anao wana na binti, si wajukuu. Wana na binti! Yeye hawakubali wajukuu. Kila mtu hana budi kuja vile vile huyo mwingine alivyokuja. Huna budi kuwa mwana au binti.

126 Kwa hiyo unaona, kuchanganya mbegu, kile kumefanya? Kanisa tu. Sisi sote tulihukumiwa kupitia Hawa, kwa kuchanganya mbegu. Hiyo ni kweli kabisa. Sisi sote hufikia mahali hapo, kupitia Hawa. Hawa alisababisha jamii yote ya

wanadamu kuanguka. Yeye na Adamu ni kitu kimoja. Yeye, ilianza na mwanamke. Itaishia na mwanamke.

127 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mtu mmoja katika yeye, aliitwa, "yule mtu wa kuasi." Wanasamehe dhambi, duniani.

128 Wakichukua fundisho lao, na kuwapa watu, nao wanakunywa hilo. Watu wa duniani, "wafalme," Biblia inasema, "wamelevya kwa mvinyo ya uasherati wake." Ni nini "uasherati wake"? Kukosa kwake uaminifu. Mwanamke anayefanya uasherati, anaishi bila uaminifu kwa mume wake. Kanisa linalofanya uasherati, huhubiri kitu ambacho si Neno la Mungu, hulifanya kanisa chotara.

129 Alifanya nini? Alizaa mabinti fulani, pia. Sasa ni nini hao mabinti, kanisa Katoliki? Luther alitoka wapi, na kuendelea, hayo madhehebu na mashirika? Unaona mahali yanapoingilia?

130 Lakini Kanisa la kweli la Mungu limejisokota miongoni mwa kila moja la hayo, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na kote kupitia pale, Kanisa halisi la Mungu, lililonunuliwa kwa Damu, kama ule ukanda mwekundu ambao wapelelezi walishushwa kwao. Wamechanganyikana, humo ndani, lakini madhehebu yao hayawezi kuwaokoa. Je, wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mmethodisti." Hilo halimaanishi chochote kwa Mungu. Wewe ni Mkristo wakati umezaliwa upya. Yeye alisababisha yote.

131 Mara nyingi, nimesikia watu wakisema, "Basi, Ndugu Branham, kwa sababu Adamu na Hawa walifanya uovu, wakalichanganya Neno la Mungu, na kutufanya tuingie katika hali hii, Mungu hana haki akinihukumu mimi. Sikuhusika nao. Sikutenda dhambi. Ilikuwa ni Adamu aliyetenda dhambi. Biblia ilisema, 'Nilizaliwa katika dhambi, nikaumbika katika uovu, nikaja duniani nikisema uongo.' Hivyo basi, mtu fulani aliniwakilisha."

132 Jamani, hili hapa wazo, huenda likakukaba roho. Mtu fulani alikuwakilisha, kama mwenye dhambi, lakini ilikuwa ni yule aliyelichanganya Neno. Basi, leo hii, ikiwa unatarajia kanisa la Kipentekoste, ama Methodisti, Baptisti, kukuwakilisha, ni neno chotara, na limehukumiwa. Umehukumiwa kwa sababu kwamba Adamu alikuhukumu. Adamu na Hawa, wakiwa mmoja, walikubali hali ya uchotara, na kuuhukumu ulimwengu.

133 Basi unasema, "Ndugu Branham, ni kwa nini mimi. . . Ni kwa nini Mungu aniwajibishe, kwa sababu mtu mmoja aliniwakilisha, halafu nife kwa sababu kwamba mtu huyo mmoja alitenda dhambi? Basi, mimi ni mwenye dhambi kwa uwakilishi." Hiyo ni kweli. Wewe ni mwenye dhambi kwa uwakilishi. Wewe kamwe. . .

134 Mungu hakuwajibishi kwa kuwa mwenye dhambi. Hakuwajibishi kwa sababu unasema uongo na kuiba, na—na—na mambo ufanyayo. Hakuwajibishi kwa kuwa mwenye dhambi.

Anakuwajibisha kwa sababu hujipi msaada mwenyewe. Kuna njia iliyoandaliwa kwa ajili yako. Unakataa njia ambayo Mungu alikuandalia, hiyo ndiyo inayomfanya Mungu kukuhukumu. Ipo njia ya kuponyokea.

135 Kuchanganya mbegu. Kuchanganya mbegu, loo, jinsi kunavyochukiza! Kuchanganya mbegu. Wanawafanya watu chotara. New York, kalibu kubwa . . . Ninao mamia ya marafiki wa thamani weusi, ambao ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Lakini katika mstari huu wa ubaguzi na mambo wanayozungumzia, kuchotarisha watu! Kitu gani? Niambie ni mwanamke mweusi yupi aliye Mkristo mzuri, aliyestaarabika, angetaka mtoto wake awe chotara, aliyezaliwa na mzungu? La, bwana. Si sahihi. Ni mwanamke yupi mzungu angetaka mtoto wake awe chotara, aliyezaliwa na mtu mweusi? Mungu alitufanya kile tulicho. Hebu tudumu kile Mungu alichotufanya. Ninaamini ni sahihi.

136 Wakati ule mzozo mkubwa ulipoibuka, kule chini Shreveport, hapa muda si mrefu uliopita, maskini yule mhubiri mweusi alisimama nje pale. Ana mahali moyoni mwangu. Akasema, "Sijaaibika kamwe kwa sababu mimi ni mtu mweusi." Kasema, "Mungu alinifanya kile nilicho, nami ninajivunia hilo. Bali," kasema, "leo hii, ninaona aibu jinsi nyinyi watu mnavyotenda. Jinsi watu wangu wenyewe wanavyotenda, inaniaibisha." Loo, jamani!

137 Tunafanya nini, marafiki? Watu wanafikiri wanajua yote kulihusu. Watu wangekuwa bora zaidi, kama ukiwaacha tu jinsi walivyo, jinsi Mungu alivyowaumba. Acha jamii ya hudhurungi ioe jamii ya hudhurungi. Jamii ya wazungu ioe jamii ya wazungu. Jamii ya weusi, jamii ya manjano, na chochote zaidi, zibaki jinsi Mungu alivyowaumba.

138 Kama ni urujuani, Mungu aliiumba, ikiwa nyeupe, acha ibaki nyeupe. Ni samawati, nyeusi, hudhurungi, chochote ua lilicho, liache.

139 Kama mahindi yalikuzwa kwa njia fulani, mahindi ya manjano, usichanganye na mahindi meupe. Ukichanganya, uyachanganye, basi hayawezi kujizaa tena.

140 Kama nyumbu alikuwa . . . ama—ama punda dume alikuwa punda dume, na punda wa kike, kwa kuanzia, acha wakae hivyo. Usiwachanganye na farasi. Unafanya haini.

141 Kuchanganya mbegu, loo, jinsi kulivyo laana. Rudi mahali Mungu alipoanzia. Hebu turudi kwenye mwanzo. Turudi mahali Mungu alipotuleta, kile tunachopaswa kuwa.

142 Nasema hili kwa heshima. Nasema hili kwa heshima. Naenda Afrika, lakini, mnajua nini, kwa ndugu yangu mweusi na dada wa thamani.

143 Mojawapo ya makosa makubwa zaidi taifa hili lililofanya, lililifanya tarehe 11 Novemba, mwaka huu. Hilo lilikuwa kosa lake kubwa, baya sana. Moja ya makosa makubwa zaidi ambalo jamii ya watu weusi iliwahi kufanya, ilikuwa ni huko chini Louisiana na huko, wakati walipompigia kura Kennedy, hivi majuzi usiku, wakamwingiza. Kwa kweli walilitemea mate lile vazi la Abraham Lincoln, ambapo damu ya chama cha Repablikan ambayo iliwaweka huru, na kumpigia kura Mkatoliki. Ambapo, Booth alimpiga risasi Lincoln. Naye akafa kwa ajili ya jamii ya watu, kuwaweka huru na kuwafanya wasiwe watumwa. Halafu, wanageuka na kumpigia kura Mwanademokrasia, na licha ya hayo, Mkatoliki. Walileta moja ya aibu kubwa zaidi waliyowahi kuleta, kwa sababu (nini?) mzungu, pamoja na elimu yake, alikuwa amewapatia kelele nyingi. Hiyo ni kweli kabisa.

144 Nina furaha sana kuna wengi wao wanajua mahali wao—mahali wanaposimama.

145 Iwe sawa na mimi nikimtemea mate Kristo, aliyeniponya na kuniokoa kutoka kuwa mwenye dhambi, na kugeuka dhidi Yake, kwa ajili ya kitu kingine, nimpe Yeye kisogo na kuondoka.

146 Loo, huku kuchanganya mbegu! Loo! U—ulimwengu unawezaje kuendelea zaidi? Si ajabu, ono la Bwana linasema hapa, kwamba, "Nililiona hatimaye likija mahali ambapo ni lundo moja kubwa tu la kuteketezwa. Lililipuliwa." Tuko njiani tukiondoka, enyi marafiki. Hakuna njia ya kuninii, hakuna njia, hakuna njia ya kuliepuka. Hatuna budi kulifikia, kulikabili. Kuchanganya mbegu!

147 Unasema, "Siwajibiki, kwa sababu Hawa alifanya hilo." Hawa kweli alilifanya. Alituwakilisha sote. Adamu alituwakilisha, huko, kama wenye dhambi. Na sisi ni wenye dhambi. Aliwakilisha asili yetu ya binadamu, iliyoanguka, kutuondoa kwenye Neno la Mungu, kulichanganya.

148 "Loo, ninajua Mungu alisema. Lakini, hakika, Mungu anaelewa ya kwamba mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpentekoste. Mungu anaelewa hayo."

149 Mungu anaelewa kitu kimoja, hicho ni Damu. Hiyo tu ndiyo anayoelewa. Anajua Damu. Hajui mipaka ya rangi. Hajui mipaka ya jamii. Kama mtu huyo ni mweusi, samawati, mweupe, hudhurungi, ama rangi yoyote aliyo, Mungu hajui chochote kuhusu hiyo. Wao ni wana na binti. Aliwafanya kama shamba Lake la maua. Anapenda kuwaona jinsi walivyo. Waache hivyo.

150 Hawa alianzisha kitu hiki kiovu, wakati alipochanganya mbegu pale na kitu hiki kingine kilichokuwa karibu na mwanadamu, ambaye angechanganyisha mbegu. Maana, nyoka alikuwa na uzao ambao daima ulikuwa "uponde."

151 Ninaichukulia upande wa imani, kwa ajili ya Wakristo wanyonge ambao hawaelewi. Hebu tuchukue imani, basi.

Semeni basi, "Kwa imani, kwa kuzalisha basi kwa imani," kama usemavyo, "Ndugu Branham."

152 Basi Hawa aliingiza theolojia yake, yeye na Adamu, na kujaribu kushawishi, mmoja kwa mwenzake, na kulirudisha nyuma. Kulaumiana, kama wasemavyo kwenye jeshi. "Mwanamke uliyenipa Wewe." "Nyoka alinidanganya."

153 "Nyoka alinidanganya." Kamwe hakumpa tofaa, kudanganya. Mnaona? Mtu yeyote anapaswa kuwa na fikira za kawaida ili kujua hilo. Lakini, "Nyoka alinidanganya," alifanya jambo la aibu.

154 Mungu alikilaani kitu hicho mpaka hawawezi kupata mfupa, katika nyoka, unaofanana na mwanadamu. Kamwe hawataupata. Wao ni wapumbavu tu, wakichimba kote. Ni hayo tu. Siri ya Mungu iko Naye. Hiyo ni kweli. "Nayo nchi ilijaa majitu."

155 Naye Josephus alisema, kwamba, yule mwanahistoria mashuhuri . . . Ungeweza kumwazia mwanahistoria, kama Josephus, akisema kwamba, '"Wana wa Mungu waliwaona binti za watu,' nao wakajisukumiza, kutoka kuwa Malaika, wakaingia katika mwili wa kibinadamu"? Mwanahistoria. Hiyo ikiwa ni hivyo, basi Shetani ni mwumba. Basi tuko wapi? Unaona? Kuna Mwumba mmoja, huyo ni Mungu.

156 Shetani hupotosha tu kile Mungu ameumba. Na uovu ni haki tu iliyopotoshwa. Ni haki kwa mume na mke kuoana, bali si kukimbia na mwingine. Unaona? Ni upotovu. Mauti ni uhai uliopotoshwa. Nalo kanisa lililopotoshwa limetolewa kwenye lile la asili.

157 Kwa hiyo, sote tumehukumiwa, na wanadamu, chini ya uwakilishi. Adamu alituwakilisha mbele za Mungu, kama wenye dhambi, wasioamini katika Neno Lake. Tumechukuliwa katika msingi huo, wasioamini Neno Lake.

158 "Loo, Mungu alisema hivyo, bali ninajua Mungu ni Mungu mwema. Hatafanya *hivyo*." Ninasikia kwa wingi sana, hilo.

159 Mungu ni Mungu mwema, lakini Mungu ni Mungu wa hukumu. Mungu ni Mungu wa utakatifu. Mungu ni Mungu wa—wa haki. Mungu ni Mungu wa hasira. Tutasimama mbele Zake wakati akiwa na hasira, Biblia ilisema hivyo, na Uwepo Wake wenyewe utakuwa Moto ulao. Hiyo ni kweli.

160 Usijaribu kumhukumu Mungu kwa hisia yetu wenyewe. Inatubidi kumhukumu Mungu kwa Maneno Yake, yale Yeye aliyosema. Usiende katika mhemuko fulani, "*Hili* ni kanisa kuu, limepitia shida nyingi," na *hili,* ni *lile*. Rudini kwenye yale Mungu aliyosema. Ninasimama mbele Zake, ninataka nipatikane bila ya hatia ya kuwahi kujaribu kuongeza kitu kimoja kwenye hilo Neno, au kuondoa kimoja. Ninataka

kuliamini tu Hilo hasa jinsi lilivyo. Wafundishe watu kulitii moja kwa moja.

161 Nayo Biblia inasema *Hili*. Siwezi kusaidia kile yeyote asemacho, sina budi kudumu moja kwa moja na Hilo.

162 Kwa kutawadha miguu, wanasema, “Ah!” Ndugu wa kipentekoste, “Ndugu! Loo, Ndugu Branham, hilo ni... Loo, tulizoea kufanya hilo.” Hebu tulifanye, bado, kama tulilifanya wakati mmoja. Yesu alililifanya, kutawadhana miguu. “Loo,” unasema, “ni hatari kwa afya. Watu wana miguu iliyokakawana.” Sijali kile walicho nacho. Huenda walikuwa nacho katika siku hizo.

163 [Ndugu Gene anasema, “Wanaponywa.”—Mh.] Naam. Naam. Hiyo ni kweli, Gene. Mungu ni mponya. Mnaona?

Wanajaribu kutafuta njia ya kuepukia.

164 Kama, kusema, “Loo, siwezi kunywea bilauri ile ile aliyoinywea mtu mwingine, isipokuwa isafishwe kwa maji moto.” Loo, jamani!

165 Ndugu yangu na dada ni ndugu yangu na dada. Amina. Mungu ndiye kinga yangu kukiwa na shida yoyote. Ninamtumaini. Hebu turudi kwenye Neno. Sijali, rangi yake, chochote alicho, ama kwamba ni mfuasi wa kanisa lipi. Ikiwa yeye ni ndugu yangu, yeye ni ndugu yangu.

166 Nitatimiza amri za Mungu. Hiyo ndiyo sababu, marafiki, inapofikia ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, sina budi kubakia hapo. Loo, hilo linaniepusha na ninii nyingi kuu... kuokoa nafsi huko nje. Hakika inaokoa, juu ya jambo hilo moja, kwa sababu ya imani ya utatu iliyokiuka mipaka.

167 Hakika, ninaamini Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, kuwa ni ofisi za Mungu; si miungu watatu, bali ofisi tatu za Mungu yule yule. Yeye ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, bali hizo ni sifa za ofisi Yake. Yeye ni Mungu, Baba, hakika alikuwa, hapo mwanzo. Yeye ni Mungu, Mwana, aliyefanyika mwili, duniani. Yeye ni Mungu, Roho Mtakatifu, aliye ndani yangu. Bali ni Mungu yeye yule, kila wakati, ofisi tatu.

168 Wakati mmoja asingaliweza kuguswa wala chochote. Kisha akashuka chini, akafanyika mwili, akachukua dhambi zangu, na kubeba dhambi zangu. Ndipo wakati aliponitakasa kwa Damu Yake Mwenyewe, ndipo Roho Mtakatifu angeweza kuingia. Basi mimi na Yeye tunaweza kushirikiana, kama tulivyofanya huko Edeni. Tu—tu—tunapendana. Yeye ni Baba yangu; mimi ni mwana Wake. Si miungu watatu. Mungu yule yule aliyeniumba, na kunipenda, akajitoa Mwenyewe kwa ajili yangu, ndiye Mungu aliye ndani yangu. Jina Lake lilikuwa ni Yesu Kristo wakati alipokuwa duniani. “Hakuna Jina jingine chini ya Mbingu lililotolewa miongoni mwa wanadamu ambapo unapaswa kuokolewa.”

169 Sasa, kama likiwaudhi rafiki zangu, siwezi kusaidia. A—afadhali nimwudhi rafiki yangu kuliko kumwudhi Baba yangu. Unaona? Yeye ni jamaa yangu, Baba yangu, Mungu. Hilo ndilo Neno Lake lisemalo.

170 Mungu, hakuwa amewahi kuniruhusu kuchanganya chochote, nikisema, "Siku za miujiza zimepita. Loo, Yesu hafanyi hivyo. Loo, hiyo huenda ikawa ni telepathia. Hiyo huenda ikawa ni kusoma mawazo. Siamini tunao manabii katika siku hizi." Biblia ilisema tutakuwa hivyo. Ninaamini Hilo.

171 Tunatafuta upako, kama vile Yohana Mbatizaji aliyejitokeza kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, anakuja kutangulia Kuja mara ya pili kwa Kristo, kama alivyofanya. Aliliahidi. "Kurejesha Imani ya watu, imrudie Mungu." Yohana alikuwa afanye nini? "Kuirejesha Imani," Imani iliyokuwa, wakati mmoja, Mbegu halisi iliyokuwa katika bustani ya Edeni. Kuliamini Neno la Mungu, mahali lilipochanganywa, na ukanisa, Yohana anakuja kulirejesha, Haleluya, kulitikisa taifa, kabla ya Siku iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana kuja. Hiyo ni ya Yohana, huduma ya Yohana, mpakwa mafuta. Tazama.

172 Pia, unasema, "Vema, basi, ni kwa nini hiyo inihukumu, kwa sababu Hawa na Adamu walifanya hili? Waliniwakilisha, kama mwenye dhambi. Siwezi kuliepuka hilo."

173 Naam, lakini, ndugu, siku moja, kulikuwa na Mmoja aliyetoka Utukufuni, tena. Loo, Yeye Ndiye ninayetaka kuzungumza juu yake, kwa yapata dakika mbili sasa. Mmoja alikuja kutoka Utukufuni, na akawa dunia. Mmoja alikuja na kuchukua umbo la mwanadamu mwenye dhambi. Alikuja kutuwakilisha, pia.

174 Naye Shetani alijaribu kumvuruga. Loo, alifanya hivyo. Kila mahali, Shetani alijaribu kumvuruga. Lakini Yeye hakuvurugika. Alibeba msalaba na kupanda juu. Amina. Shetani asingeweza kumvuruga. La, la. Alikuwa ni aina tofauti ya Adamu. Yeye alitoka Utukufuni, kutuwakilisha.

175 Nini? "Vema," Adamu akasema, "kama mke wangu amesema hivyo, nadhani hiyo ni sawa. Vema, alisema alipata ufunuo, na *hivi* ndivyo inavyopaswa kuwa. Ninajua Mungu anasema ni *Hivi*, lakini mke wangu alisema . . . "

176 Hivyo ndivyo ilivyo na mshiriki wa kanisa la mahali hapo leo hii. "Loo, ninajua Biblia inasema *Hivyo*, lakini kanisa langu linasema *hivi-na-hivi*." Loo, ewe maskini, mnafiki mwenye mashaka! Hivi huoni?

177 Mungu alisema, "Acha Neno Langu liwe kweli, na neno la kila mtu liwe uongo." Mchukue Mungu katika Neno Lake. Ni Neno la Mungu! . . . jali kile mke wangu alichosema, kile kanisa langu lilichosema. Ni kile Mungu alichosema.

178 Hivyo basi, walipomwona aliyemsukuma mke wake, Hawa, wakati alipokuja kukutana na Yesu, ilisema, "Loo, naam, imeandikwa, kwamba—kwamba, 'Atawapa Malaika agizo juu Yako, usije wakati wowote ukajikwaa kidole chako kwenye jiwe, watakubeba.'"

"Naam," Yeye akasema. "Na pia imeandikwa . . . "

179 Loo, asingeweza kumvuruga. Yeye alikuwa ni Mungu, aliyefanyika mwili. Alikuwa Mwokozi wangu na Mungu wangu. Asingeweza kumchanganya.

180 Alifanya nini basi? Aliukumbatia msalaba. Na hapo msalabani Yeye alikufa, kwa ajili yangu mimi na kwa ajili yako, na kwa ajili ya ulimwengu, ili aweze kurejesha tena, kwa Mungu, (kitu gani?) wana na binti, kama katika bustani ya Edeni, kabla hawajachanganyikiwa katika theolojia.

181 Ee Mungu, laiti watu wangaliweza tu kuona hilo! Laiti ningaliweza tu kushindilia hilo ndani ya watu!

182 Yesu alikufa, ili aweze kutoa watu kwenye upuuzi huu wa kanisa chotara, ili aweze kuziondolea nia zenu na imani mbali na yale mwanadamu aliyosema, kuzirudisha kwa yale Mungu aliyosema.

183 Si imani chotara, "Vema, labda siku za miujiza zimepita. Labda hayo hayatatendeka."

184 Loo, ndugu, Mungu alisema yanatukia, na hilo latosha. Hiyo ni sikuzote. Mungu alisema hivyo. Yesu alikufa ili aweze kuzaa tena. Loo, Haleluya! Damu pekee ndiyo iwezayo kufanya hayo. Ni kupitia kemia ya Damu ya Yesu Kristo pekee, inaweza kuzaa tena, mtu ambaye hatatofautiana Neno moja kutoka kwa yale Mungu aliyosema.

185 Hawa alionyesha udhaifu wake, kanisa, alionyesha yale aliyofanya. Akasema, "Vema, labda uko sawa. Labda Mungu hataniwajibisha. Maana, mimi sininii tu . . . Vema, kama nikininii tu . . . Loo, inaleta tofauti gani, mradi tu nimebatizwa? Unaona? Inaleta tofauti gani, mradi tu mimi . . . " Loo, wewe . . . La. Hiyo inaonyesha unahitaji kuzaliwa kwingine.

186 Hiyo inaonyesha kwamba Kitu fulani inabidi kikurudie, kukuleta kwenye Imani katika yale Mungu aliyosema. "Hata nukta moja wala yodi moja haitapita kutoka kwenye Neno la Mungu, hata yote yatakapotimia. Neno la kila mtu na liwe uongo, na Lake liwe kweli."

187 Kristo alikuja ili aweze kuzaa tena, kwa Roho Mtakatifu. Loo, ndugu, tunapoketi pamoja sasa mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, Roho Mtakatifu akipumua juu yetu, kama tulivyo sasa. Akizalisha tena, akiondolea mbali takataka za theolojia, kuondolea mbali takataka za ulimwengu, mafundisho ya kujibunia, "kuwa na mifano ya utauwa, huku wakikana

Nguvu zake." Kuzalisha tena kuwa Imani isiyoghoshiwa katika Mungu. Yesu alisema . . .

188 Shetani alisema, "Loo, ninajua imeandikwa. Lakini, unajua, imesemekana Wewe utaninii . . . "

Yeye, Yesu, kasema, "Pia imeandikwa pia . . . Pia imeandikwa . . . "

189 "Naam, imeandikwa kwamba Yeye atafanya *hili*. Na Wewe utageuza ninii . . . Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, unaweza kufanya mwujiza hapa mbele zangu, na kugeuza mawe haya yawe mkate. Hebu nikuone ukifanya hivyo." Angekuwa anamjali Shetani.

190 Unaona werevu wa Mungu hapo? "Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate pekee." Mwone Yeye, moja kwa moja na Neno. Yeye kamwe . . . Alimshinda Shetani, kila wakati, moja kwa moja kwenye Neno. Alidumu na Neno.

191 Basi Yeye akija kutuzaa sisi turudi kuwa wana na binti za Mungu, kama tulivyokuwa kwenye mwanzo, tunawezaje kuliondokea Neno basi? Tunawezaje kufika popote mpaka turudi kwenye Neno? Loo, natumaini kanda hii inayoenda kwa watu, nanyi mnanisikiza, kote ulimwenguni, kwamba mtatambua hilo. Tuna . . . Ikiwa sisi ni wa Kristo, tumezaliwa na Kristo. Inatubidi kurudi kwenye Neno.

192 Kamwe hatutaweza kuwaelimisha watu kuingia ndani Yake. Huenda tukajenga makanisa makubwa, ndugu zangu, katika ulimwengu huu. Huenda tukajenga na kuwa na mipango mikubwa ya elimu. Tumejaribu kufanya hivyo. Inatengeneza wahuni.

193 Wahalifu wengi zaidi wanatoka wapi? Kutoka kwenye, si maeneo ya watu wasioelimika, bali kutoka kwa walioelimika, kutoka kwenye jamii na ki—ki—kizazi cha wenye vyeo, wenye elimu.

194 Si muda mrefu uliopita, niliposimama na wakala wa FBI, naye akaonyesha, ukutani, na akasema, "Ninathamini mahubiri yako." Akasema, "Ulisema kwamba si tabaka la watu maskini, wanaozalisha, mtu maskini ambaye hajui mengi sana. Hao wavulana, kidogo wanaogopa kucheza nalo. Bali ni aina hizi wanaofikiria wanaweza kumshinda akili huyo mjanja mwingine. Wanaona mahali alipofanyia kosa lake, na kulijaribu." Alienda moja kwa moja kwenye vizimba na kuonyesha visa vyote vya uhalifu wa vijana kote katika taifa. Na asilimia themanini yao, au zaidi, zilitokana na ujirani wa kikabaila, werevu, wenye akili.

195 Angalia mwanzo, sasa, inaonyesha kwamba hao ni wana wa—wa—wa Kaini. Waangalie watu wa Kaini. Watu wa Kaini walikuwa ni kitu gani? Wafuatilie, hadi kwenye ukoo, ukishuka kupitia watu wa Kaini. Walikuwa kitu gani? Walikuwa werevu, wanasayansi, madaktari, watu wenye vyeo, wa kidini, watu wa

tabaka la juu. Walivumbua jinsi ya kufua vyuma mbalimbali, jinsi ya kujenga majengo mazuri. Walikuwa ni wanasayansi.

196 Hao wengine walipitia nini? Vibarua wa shamba, wakulima, wachunga kondoo, kadhalika. Mnaona hilo?

197 Hebu liangalie, leo hii, hawa wenye akili. Wamelichanganyisha ndani ya makanisa, hata kanisa halitaki mtu duni asiye na elimu, ambaye kweli anampenda Bwana, aje hapo. Pengine mhubiri aseme jambo, wanasema, "Amina," watamtoa nje ya mlango. Hawawataki kwenye kusanyiko lao, kama hawezi kuvalia vizuri, na kuvalia kama kina Jones ama mtu mwingine. Mnaona? Ha—hawawataki mle ndani, kama hawawezi kuendesha gari zuri, wanaendesha maskini vikorokoro mbele ya kanisa. Ndugu! Ndugu, loo, hivi huwezi kuona?

198 Na wengi wa watu siku hizi hata hawatawakaribisha watu weusi makanisani mwao. Ee Mungu, warehemu wanafiki kama hao.

199 Mungu, ninaitaka, daima. Mradi tu nina kanisa, milango imefunguliwa kwa yeyote atakaye. Sijali kama utakuja kwa mkokoteni, wewe njoo. Wewe njoo. Sijali kama unavaa surupwenye. Nitasema jambo moja. Wewe kuwa sawa na Mungu, na jozi ya surupwenye inaweza kuketi chini karibu na suti rasmi, nao watakumbatiana kwa mikono mmoja na mwenzake, na kuitana mmoja na mwenzake "ndugu." Hakika watafanya! Hakika itakuwa hivyo. Nguo ya kaliko inaweza kuketi karibu na nguo ya hariri, na kukumbatiana na kusema, "Dada." Naam. Hukufanyia jambo fulani. Linazalisha tena.

200 Basi tunafanya nini sasa? "Tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu." Sio kuchukua theolojia yetu, bali kumwacha Roho Mtakatifu atuzae tena kuwa wana na binti za Mungu.

201 Neno *kutahiri* linamaanisha nini? [Ndugu mmoja anasema, "Kukatilia mbali."—Mh.] Stefano alisema . . . Hiyo ni kweli. "Kukatilia mbali nyama ya ziada." Unaona? Kukatilia mbali ya ziada, sehemu isiyohitajika. *Tohara*, "kukatiliwa mbali." Sasa, katika Agano la Kale, ninii, mwanamume pekee ndiye angeweza kutahiriwa, nyama ya ziada ilikatiliwa mbali.

202 Sasa, kile Roho Mtakatifu afanyacho, katika siku za mwisho, hukatilia mbali ya ziada, hukatilia mbali theolojia ya ulimwengu, hukatilia mbali mafundisho ya wanadamu, hukatilia mbali kutokuamini kwote, hukatilia mbali kila kitu. Stefano alisema, "Loo, enyi msiotahiriwa mioyo wala masikio. Kwa nini mnampinga Roho Mtakatifu siku zote? Kama baba zenu walivyofanya, nanyi ni vivyo hivyo."

203 Hapo ndipo ilipo, rafiki. Inakubidi kuondokea, tuseme, "Vema, sasa, nilisikia hotuba hivi majuzi usiku, kasema, 'Hao waponyaji wa Kiungu, wao, afadhali uwaangalie.' Si waponyaji

wa Kiungu. Ningewaangalia pia. Bali ninaangalia Neno la Mungu, kile Hilo lisemacho. Ninachukua Neno. Neno lilisema hivyo. Mnaona?

204 "Ah, inakubidi kuwaangalia hao watu wanaoamini katika kunena kwa lugha, kwa sababu hiyo ilikuwa ni siku nyingine. Hao si kitu ila pepo."

205 Neno lilisema nini? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, hata ukamilifu wa dahari. Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Agizo la mwisho la Yesu kwa Kanisa Lake.

206 Roho Mtakatifu anajaribu kufanya nini leo hii? Kukatilia mbali kutokuamini huko kwote. "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Kujaribu kurudisha watu kwenye Neno lisiloghoshiwa, ambapo Mungu alisema, kama ilivyokuwa kule Edeni kabla ya theolojia kuongezewa, lirudisheni Hilo jinsi lilivyokuwa katika Edeni, wakati mwanadamu alipotembea na Mungu. Naye akasema... Kama mti haukuonekana kuwa sawa, *hapa*, alisema, "Ng'oka na usonge huku." Upepo ulikuwa ukivuma. Kasema, "Amani, tulia," nao ukakoma. Chochote alichokuwa, yeye aliwatawala wanyama wote. Kila kitu duniani, kilikuwa chake. Alikuwa ni mungu juu ya dunia. Alikuwa na mamlaka ya utawala ndani yake.

207 Mtu alishuka kutoka Mbinguni, katika mchafuko huu wote, na kuthibitisha kwamba huo ulikuwa ni mpango wa Mungu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Basi alifanya nini? Alikufa, ili sisi tuweze kurudi na kutakaswa kupitia haki ya Damu Yake. Na Yeye anatuwakilisha asubuhi ya leo. Haleluya!

208 Sasa, kwenu ninyi mnaosema ni kosa kuwakilishwa na Adamu, kama mwenye dhambi, vipi kuhusu, kupitia uwakilishi, tuna wokovu, pia? Huwezi kujiokoa mwenyewe kuliko vile ungeweza kuchukua ugwe wa viatu vyako na kuruka nao kupita mwezi. Huwezi kamwe... Umezaliwa katika dhambi. Wewe ni haini, kwanza kabisa, kila mmoja wetu, wala tusingeweza kujisaidia wenyewe. Basi tutapataje kuokolewa? Mmoja alikuja kutuwakilisha.

209 Yesu, Yeye alikuja kutuwakilisha mbele za Mungu, kama wana na binti za Mungu. Naye alituma Roho Wake Mtakatifu sasa, kwamba Yeye anaatamia mahali hapo, akijaribu kuturudisha kwenye Kuzaliwa, ili tuwe... tuifie nafsi yetu, na kuzaliwa upya, tena, kuwa wana na binti za Mungu, kumwamini Mungu kwenye Neno Lake, kuliamini Neno la Mungu.

210 Sasa, iwapo tuna hukumu kwa uwakilishi, sisi pia... Tunakuwaje na hukumu? Kwa sababu ya kuchanganya mbegu. Kuingiza ndani, ulimwengu, pamoja na vitu vya Mungu, hivyo ndivyo tulivyo navyo.

211 Sasa, tunapataje kamwe kuondokea huko kuchanganya mbegu? Achana na takataka hiyo iliyochanganyiwa mbegu. Rudi kwenye Hili, kwenye Neno la Mungu kuwa Kweli; neno la kila mwanadamu uongo. Alilosema Mungu ni kweli. Dumu moja kwa moja na Hilo, hukuzaa moja kwa moja tena kurudi kwenye Hili. Ipo njia iliyoandaliwa, Mtu aliyesimama kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, asubuhi ya leo, kukuwakilisha.

212 Baba yako na mama walikuwakilisha, kama Adamu na Hawa. Na hiyo ni kweli. Ulipozaliwa duniani, ndoa takatifu, ilikusudiwa na Mungu kuwazaa watoto. Sasa umerudi moja kwa moja mahali pale ulipokuwa katika bustani ya Edeni, kama vile Adamu na Hawa, enyi wana na binti za Mungu. Mmerudi moja kwa moja kwenye miti miwili. Mmoja wayo ulikuwa ni mti wa maarifa, na huo mwingine ulikuwa ni Mti wa Uzima.

213 Sasa, mnataka kuendea njia ya kisayansi ya kuchanganya mbegu? Angalieni mlipofikia. Ni nini . . . Ni machafuko ya jinsi gani mwanadamu amejiingiza kwa kuchanganya mbegu? Ni machafuko ya jinsi gani aliyojiingiza ndani, kwa maarifa yake mwenyewe? Badala ya kuwa tu mtoto, kwa unyenyekevu, na kumtegemea Mungu, yeye anajaribu kuchukua sayansi na kupasua atomu. Angalia mchafuko aliomo sasa hivi. Mungu humwacha tu ajiangamize mwenyewe. Hivyo tu.

214 Mwanadamu alijiangamiza mwenyewe, hapo mwanzo, akajitenganisha na Mungu, na ushirika, kwa mti wa maarifa. Aliuacha Mti wa Uzima, kuula mti wa maarifa. Ondokea mti huo chotara. Ingia hapa kwenye Tunda la asili lililo na Uzima ndani Yake. Mle Yeye.

215 Yesu alisema, "Mimi ndimi Mkate wa Uzima ulioshuka toka kwa Mungu Mbinguni. Baba zenu walikula mana jangwani," pasipo kuchanganywa na imani, mnaona, "walikula mana jangwani, nao wote wamekufa. Bali Mimi ni Mkate wa Uzima ulioshuka kutoka kwa Mungu Mbinguni. Yeye aulaye Mkate huu yuna Uzima wa Milele. Nitamfufua katika siku za mwisho. Hataangamia kamwe; anao Uzima usio na mwisho."

216 Hebu turudi kwenye Mti, asubuhi ya leo. Hebu tuyaondokee yale mwanadamu asemayo. Hebu tuyaondokee yale—yale—yale makanisa yasemayo. Hebu turudi na kuichukua Biblia, na kuiamini Biblia. Tu—tumechelewa kupita kiasi, sasa, kuanza kuzozana. Unaona?

217 Kamwe hatutakuwa na madhehebu zaidi kuinuka. Ninaweza kuthibitisha hilo sasa, kwenye kipindi cha nyakati za kanisa. Kamwe hatutakuwa na mengine yakiinuka, madhehebu. Wakati wa Kanisa la Laodikia utakuwa tu ni Wapentekoste wakijiundia madhehebu na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, namna hiyo. Lakini kamwe hakutakuwepo tena na miamsho kuanza, itakayoipiga nchi. Wale wachache tu waliosalia, Kanisani, watawavuta wale wanaopaswa kuingia.

Kwa kuwa ni . . . Biblia inasema, nyakati za kanisa zinamalizika katika hali ya "uvuguvugu". Hiyo ni kweli. Kwa hiyo haina budi kuja kwa njia hiyo.

218 Sasa, kwa wote, hebu tuondokee huku kuchanganya mbegu. Hebu turudi kwenye lile Tunda halisi, la asili. Hebu turudi mahali ambapo Mungu alituumbia, kama wana na binti za Mungu, kutegemea yale Mungu aliyosema. Basi usichukue neno la mwanamke, la kuchanganya mbegu. Mnaona jinsi ya kawaida na ya kiroho zinavyofananishwa?

219 Mliona ono langu lililoandikwa hapa, kwamba lilikuwa ni nini, jinsi wanawake wangepewa haki ya kupiga kura? Ni kitu gani kilichoharibu taifa hili? Sasa, sikilizeni. Si nyinyi wanawake Wakristo. Wanawake ndio uti wa mgongo wa taifa lolote. Ukivunja umama, basi umevunja taifa, kwa kuanzia. Imekuwa hivyo, kote katika historia.

220 Wanawake wa Marekani ni nini? Ilikuwa kwamba, tulienda Paris, kupata mitindo. Sasa Paris huja huku kuchukua mitindo, kwa ajili ya njia yao ya maisha iliyo chafu, ya utovu wa adabu; wanakuja kwetu, kuchukua mitindo. Ni nini ilitendeka? Ibilisi amewavua nguo wanawake wetu. Wanavua nguo zao. Kila mwaka, wanavua zaidi kidogo.

221 Wananyoa nywele zao, ambalo, Mungu anasema, "Ni kosa." Wanavaa maskini nguo hizi ndogondogo, ambazo Biblia ilisema, "Ni chukizo mbele za Mungu, kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume." Na sasa huwezi kujua kama wao ni wanaume au wanawake. Wanavuta sigara! Chotara, ni kweli. Chotara, hata hawajui kama wao ni wanaume au wanawake. Hiyo ni kweli. Ni vigumu kujua wao ni wa jinsia gani, kwa kuwatazama na kuwasikiza. Hiyo ni kweli, rafiki.

222 Sisemi hilo kuwahusu nyinyi, wanawake Wakristo. Sauti yangu inaenda kote, mataifa mengi.

223 Lakini, ni chotara. Hii Marekani imehukumiwa. Basi lilifanya nini, kulingana na ono? Lilimchagua mtu asiyestahili. Sijui ni muda gani itakaochukua kumalizika, bali itamalizika, siku moja. BWANA ASEMA HIVI. A-ha. Itamalizika.

224 Liko katika njia yake ya kuanguka sasa. Halitawahi kurudi tena. Limekwisha. Hiyo ni kweli. Limekuwa limekwisha tangu 1956, wakati lilipohukumu na kurudi kwa Mungu, tangu nyakati za miamsho mikuu.

225 Sasa wakati umewadia, nadhani, kwetu kufunga, kwenye wakati huu, tuwe na mstari wa maombi kwa ajili ya wagonjwa.

226 Sasa, mnaamini kwamba ibilisi amewachotarisha watu, mataifa? Ninii . . . Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika amewachotarisha. Kuwachotarisha makanisa mpaka tumekuwa mafundisho ya sharti ya kujibunia badala ya watumishi wanaomcha Kristo.

227 Mnaona ni kwa nini ninakemea, na kutikisa, na kugonga, kwa nguvu niwezavyo, dhidi ya makosa? Ninawezaje kufanya chochote kingine, wakati hapa Neno linasema hivyo, na Roho Mtakatifu, "Ingia ndani Yake"?

228 Ninasema, "Bwana, ninahubiri. Wanavalia tu vile vile. Wangali wanafanya jambo lile lile walilofanya siku zote."

229 "Lihubiri Hilo, kwa vyovyote vile, endelea tu kusonga. Sauti yako i—inarekodiwa." Kwenye Siku ya Hukumu, hakutakuwa na u—udhuru wowote wakati huo, maana umelisikia Hilo. Unaona? Hiyo ni kweli. Umelisikia Hilo.

230 "Imani chanzo chake ni kusikia," na kusikia kile kanisa lisemacho? Hilo halisikiki kuwa sahihi, sivyo? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] "Kusikia Neno la Mungu," kukurudisha kwenye Imani katika Mungu!

231 Sasa, unapokuja, asubuhi ya leo, tunataka kuomba. Nasi tunataka kuomba kwamba Mungu atawajalia mweke kando kila kitu. Labda Ujumbe huu mfupi utaondolea mbali huko kuchanganya mbegu ndani yako, ukurudishe kuwa mtumishi mnyenyekevu, uje na kusema, "Ninamwamini Mungu."

232 Daima wameshangaa. Ninaweza...Nitasema jambo hili. Lisikizeni. Unasema, "Ndugu Branham, huduma yako haina kifani, popote ulimwenguni, kwa mambo yake ya kimbinguni." Watu mashuhuri, ningeweza kutaja majina yao, haikuwa kwa ajili ya kanda hii, mniite, "Njoo, uambatane nao." Kasema, "Huduma yako ndiyo kitu pekee kitakachookoa ulimwengu."

233 Ni kwa nini hiyo haiko mahali pengine? Rudi kwenye Neno. Mungu anaweza tu kujenga juu ya msingi huo. Basi, ikiwa nimekosea kabisa jinsi ninavyobatiza watu, na jinsi ninavyozungumza juu ya Roho Mtakatifu, na mambo ninayofanya, basi ni kwa nini Mungu anayaheshimu? Toa kitu kama hayo. Mnaona? Ni kwa nini? Sisemi hilo kwa ajili yangu mwenyewe; hilo lingekuwa kosa. Bali ninajaribu kusema, kwa sababu ninasimama juu ya Kweli, Neno, na Neno pekee. Kupaa juu, na kutengeneza vitu vikubwa, na mahali mashuhuri, ambapo hapana maana yoyote kwa Mungu, hata kidogo. Ni kudumu na hilo Neno, na Mungu akifanya kazi ndani ya Neno hilo, akithibitisha Neno hilo, akidumu Nalo, ishara ya Mungu aishiye miongoni mwetu.

234 Mnataka kuwa hivyo? Mnataka ulimwengu wote uoshwe na kuondolewa kwenu? Loo, jamani!

235 Enyi watoto wadogo, Mungu awabariki. Ninatarajia kuishi Milele pamoja nanyi. Ninatarajia kuwa huko katika—katika Edeni kuu, pamoja nanyi, siku moja. Basi nitakapofika Huko...

236 Nilikuwa na ono, muda si mrefu uliopita. Mlisikia habari zake. Niliangalia Kule, nikaona watu hao wote Kule. Kulikuwa

na mamilioni yao. Nami nikasema, “Unamaanisha Yeye ananijia . . . ”

“Naam. Na kisha tunarudi na wewe.”

Nikasema, “Vema, hivi inabidi kila mhudumu kusimama namna hiyo?”

“Naam, bwana.”

“Kila mhudumu kusimama kwenye huduma yake, pamoja na kusanyiko lake?”

Kasema, “Naam, bwana.” Malaika huyu, aliyekuwa akizungumza nami, alisema hivyo.

Nami nikasema, “Basi itambidi Paulo kusimama, pia?”

“Paulo hana budi kusimama pamoja na kizazi chake.”

237 Nikasema, “Basi ninajua niko sawa, maana nilihubiri, Neno kwa Neno, jambo lile lile alilohubiri.”

238 Na niliposema hivyo, mamilioni wakasema kwa sauti kuu, “Hapo ndipo tunapoegemea,” amina, “juu ya hilo Neno, hilo Neno!” Haijalishi ni kitu gani, “Hilo Neno!”

239 Hiyo ndiyo sababu ninawashurutisha watu, waje, kama itakavyokuwa asubuhi ya leo, wengine wao wakibatizwa upya, tena. Paulo alifanya hivyo.

240 Paulo alikutana na watu ambao walikuwa tu na furaha sana na kujazwa na wema wa Mungu na kadhalika, wakipaza sauti na kumsifu Mungu, na kuwa na mkutano mzuri. Akasema, “Lakini je, mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Matendo 19.

241 Wakasema, “Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu yeyote.” Kasema, “Sisi ni Baptisti tu,” kwa maneno mengine. Unaona? M—mchungaji wao alikuwa mhubiri wa Kibaptisti, kweli kabisa, alikuwa ni mwanasheria aliyeongoka. Nanii wa Kibaptisti . . .

Paulo akasema, “Je, mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wakasema, “Hata hatujui kama kuna Roho Mtakatifu.”

242 Akasema, “Basi mlibatizwaje? Mlibatizwa kwa kitu gani? Vipi? Namna gani? Kitu gani?”

“Tumebatizwa na Yohana.”

“Hiyo haitafanya kazi tena.”

Kasema, “Tulibatizwa na Yohana.”

243 Akasema, “Yohana alibatiza tu kwa toba.” Kiasi kile tu cha maji unachoweza kuwaweka chini yake, unaona, “kwa toba.” Si kwa “ondoleo la dhambi,” kwa sababu Dhabihu haikuwa imechinjwa bado. Kasema, “Kwa toba, akisema ya kwamba mnapaswa kumwamini Yeye aliyekuwa aje, ama hata Yesu Kristo.”

244 "Basi waliposikia haya, waliingia moja kwa moja majini wakabatizwa, tena, katika Jina la Yesu Kristo," kile Biblia.

245 Naye Paulo, katika Wagalatia 1:8, alisema, "Ikiwa Malaika kutoka Mbinguni. . ." Sasa sikilizeni. Ni kitu gani mimi. . . Kurudi, kitu hiki chotara, kiondokeeni. "Kama Malaika kutoka Mbinguni akija, ahubiri injili yoyote nyingine mbali na Hii ambayo nimewafundisha," Paulo, akiwabatiza watu upya, tena, "na alaaniwe." Achana na, mhubiri, au askofu, au papa, au kasisi. Ikiwa Malaika, Malaika anayeng'aa akishuka kutoka Mbinguni, na kusema chochote kinyume na yale aliyosema, na alaaniwe.

246 Tutaikabili namna gani, wapendwa? Sio tu. . .Sasa, huenda ukabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, na moyo wako una giza kadiri uwezavyo kuwa. Huo haukuokoi. Lakini ni hatua moja sahihi. Unaokolewa kwa imani yako, kupitia Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Lakini unapofikia mahali hapa na kuona Hili, halafu ulikatae, basi unarudi nyuma.

Hadithi hii fupi. Ninafunga. Nimeisimulia hapo kabla, labda hapa.

247 Kasisi wa jeshi wakati mmoja alisema walimwita ndani mahali jamaa fulani alikuwa amepigwa risasi kwa bombomu naye alikuwa yuafa. Akasema, "Wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Nilikuwa."

"Ulikuwa?" Akasema, "Ulimwacha wapi Kristo?"

Akasema, "Sikumbuki."

248 Kasema, "Afadhali uanze kutafakari, kwa sababu mapafu yako yanajaa damu." Kasema, "A—afadhali uharakishe. Kwa sababu wewe. . .Moja kwa moja chini ya mapafu yako, umepigwa risasi."

Akasema, "Ninajua hilo."

Kasema, "Unakufa."

Kasema, "Naam."

Kasema, "Na wakati mmoja ulimjua Kristo?"

"Naam."

249 Kasema, "Sasa fikiria, kwa nguvu sana. Maana, huna. . ." Kasema, "Kapteni, una muda mfupi tu sasa. Fikiria." Kasema, "Fikiria kwa nguvu sasa. Ulimwacha Kristo wapi?"

250 Na alipopambana, kupambana, akijaribu kukumbuka. Moja kwa moja tabasamu likaja juu ya uso wake. Kasema, "Ninakumbuka. Ninakumbuka."

251 Hilo ndilo likupasalo kufanya. Kumbuka, unapokuja kinyume na Kweli ya Mungu, utamwacha papo hapo. Utamwacha papo hapo. Unaona? Wala haitakufaa kitu kwenye njia *hii*, kwa sababu huna budi kufikia *Hili*. Uko katika njia

ya mchepuo, wakati wote. Sisemi wewe si Mkristo, lakini uko—uko—uko kwenye njia ya mchepuo. Walikuwa ni Waisraeli, bali si wote waliokoka. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Uko katika njia ya mchepuo, moja kwa moja basi. Wewe rudi kwenye Hilo.

Ndipo kasisi wa jeshi . . . Kasema, "Ninakumbuka."

252 Kasema, "Anzia moja kwa moja hapo." Hapo ndipo inakubidi kuanzia, asubuhi ya leo, mahali ulipopotezea mwelekeo.

253 Akasema, "Sasa ninalala usingizi. Ninaomba Bwana ailinde nafsi yangu. Kama nitakufa kabla ya kuamka, ninaomba Bwana aichukue nafsi yangu." Ndipo akafa. Mahali alipomwacha Kristo ilikuwa ni kwenye kitanda cha mtoto.

254 Huenda ulimwacha kwenye ubatizo. Huenda ulimwacha kwenye Roho Mtakatifu. Huenda ulimwacha mahali pengine. Popote ulipomwachia, usichukue takataka hii ya kuchanganya mbegu ya kanisa. Kuna Mtu wa kukuwakilisha, asubuhi ya leo, kwa ajili ya wokovu.

255 Haikupasi kuwa mwenye dhambi. Haikupasi kuwa hivyo. Wewe ni mwenye dhambi, ikiwa ndivyo ulivyo. Mungu hakuwajibishi kwa kuwa mwenye dhambi. Hatakuhesabia kuwa . . . wajibu tangu sasa na kuendelea. Bali atakuwajibisha ikiwa utakataa Hili. Hatakuwajibisha kwa sababu labda, katika wakati uliopita, kwamba hukujua tofauti na ubatizo wa maji, na kupokea Roho Mtakatifu, na nguvu za Mungu. Huenda asikuwajibishe kwa hilo. Huenda hukuwa umelisikia Hilo hapo kabla. Bali, tangu hapa na kuendelea, unajua bora zaidi. Rudi kwenye Neno. Rudi kwa Mungu.

Na tuombe sasa. Basi wewe wazia Hilo, tunapoomba.

256 Bwana, nikijua kwamba mimi ni mwanadamu anayepatikana na mauti, na hivi karibuni nitaondoka. Siku zangu zinakuwa nyingi sasa. Hivi karibuni nitakuwa na miaka hamsini na miwili katika dunia hii. Bwana, ninataka kuwa mwaminifu. Ninataka kuwa mkweli, hadi mwisho. Kote ulimwenguni, mataifa mengi, mengi, watu, rangi, jamii, nimeona kanuni nyingi za imani, na kuwaona, jinsi wanavyozichanganya, na maskini mizozo yao mbalimbali na mahangaiko. Wakati, katika sehemu hizo, wapo watoto wengi wa kweli, wanaume wengi na wanawake katika sehemu hizo, huko kwenye uwanja huo wa kichotara huko, ambao kwa kweli hawataki kuwa huko. Wanafikiri wanafanya mapenzi ya Mungu.

257 Ninakuomba Wewe, Baba, asubuhi ya leo, kuondolea mbali mashaka yote kutoka kwenye kundi langu dogo hapa leo, na kutoka kwa wale ambao watakuwa wakisikiliza kanda, kwamba Wewe utaondolea mbali kanuni za imani za kujibunia. Kama vile Yesu, wakati alipokuja kwa mara ya kwanza, aliwakuta wakifundisha mambo ambayo "hayakuwa hivyo tangu mwanzo," tangu mwanzo. Wakati, Mungu alilifanya

safi na lisiloghoshiwa. Lakini mwanadamu alikuwa amefanya, alichukua Neno la Mungu na kulitangua, kwa kufundisha kanuni za imani za wanadamu. Baba, ndivyo ilivyo sasa, karibu na Kuja kwa Yesu, tena.

258 Kama tu Mzabibu. Mzabibu ukichipusha tawi, nalo tawi hilo lilikuwa tawi la kipentekoste, lililojazwa na Roho Mtakatifu, na ishara na maajabu, matunda yalifuata tawi hilo. Mzabibu huo ukipata kuchipusha tawi jingine, litakuwa ni tawi aina ile ile. Tunajua hilo, Baba, kwa maumbile yenyewe. Bali tunajua ya kwamba Wewe unaweza kupandikiza tunda lolote linalohusiana na hilo, katika Mzabibu huo, nalo litaishi kwa Mzabibu huo.

259 Nasi tunajua ya kwamba tunaweza kuchukua mchungwa, na kukuza matunda jamii ya chungwa, ya aina tofauti, saba au manane. Tunaweza kuweka malimau juu yake. Sisi . . . Litakuwa moja kwa moja ndani, maana ni tunda jamii ya chungwa. Utakuza balungi, na mengine mengi, na chenza, na matunda mengine mengi jamii ya chungwa. Lakini mti huo ukipata kuchipusha tawi lake wenyewe tena, litakuwa ni chungwa, Bwana. Litakuwa kama la kwanza lilivyokuwa.

260 Nasi tunaamini kwamba kutakuwa na Kanisa, katika siku hizi za mwisho, ambalo litapokea mvua ya masika na ya vuli pia. Litatapakaa kote ulimwenguni, katika wakati huu wa Laodikia. Litakuwa ni Kanisa ambalo limeitwa likarudi kwenye Imani ya asili katika Mungu. Litakuwa ni Kanisa ambalo litakuwa na Yesu Kristo akitembea ndani Yake, akijidhihirisha Mwenyewe. Sauti ya Mfalme itakuwa ndani Yake.

261 Mungu, jinsi ulivyoanza, wakati baada ya wakati! Na jinsi walivyouchukua ule Mzabibu, na kuupandikiza Mle, nao unanawiri Kwalo, chini ya jina la Ukristo, huku ungali unazaa fundisho ambalo halikufundishwa hapo mwanzo. Ee Mungu, jinsi tu—tunavyosikitika kwa ajili ya hilo, Bwana. Hatujui la kufanya.

262 Bali, asubuhi ya leo, ninaomba ya kwamba Wewe utaondoa mioyoni mwetu chochote kilichobuniwa na wanadamu. Chukua na uweke mioyoni mwetu, Bwana, Neno la kweli la Mungu.

263 Ninajiandaa kuwaombea wagonjwa, Bwana. Ninawezaje kushuka huko chini na niwe na shaka moyoni mwangu, kwamba Mungu hatajibu maombi yangu? Basi, Baba, mwenyewe, ningekuwa mnafiki. Mungu, kama kuna chembe yoyote ya shaka moyoni mwangu, unisamehe hilo sasa, Bwana. Ikiwa kuna chochote ambacho nimefanya au kusema, ambalo ni kosa, nisamehe.

264 Nijalie niingie katika kile kilicho Kweli. Pia, Baba, ninajua Neno Lako ni Kweli. Ninajaribu kudumu kwenye hilo Neno. Nimechanganywa, Bwana, huko nyuma, na kwa kuzaliwa kupitia vizazi vyangu, mpaka ninajua akili yangu imevurugwa.

Lakini, hata hivyo, ninaweza kuangalia hapa chini na kuliona Neno. Ninajua ni Kweli.

265 Ninatamani kuwa Huko, Bwana. Ninashikilia hiyo nanga, huko kwenye Mwamba. Dhoruba zinaniyumbisha huku, na huko, na kote, bali nanga yangu inashikilia. Ni katika Kristo na ndani ya Neno Lake.

266 Ninaamini Neno Lako ndilo Kweli. Nisaidie, Bwana, nisipatane kamwe juu ya chembe Yake hata moja, bali kuendelea moja kwa moja na upendano wa kiungu, mikono yangu ikiwakumbatia watu wote, jamii zote, rangi zote, kanuni zote za imani, madhehebu yote, nikawavuta kwenye Mwamba. Tujalie, Baba.

267 Waponye wagonjwa wote na wanaoteseka. Warudishe kuwa aina ya watu wa uamsho, wa mtindo wa kale, leo hii. Warudishe kwenye pentekoste asili. Warudishe kwenye baraka. Warudishe kama pentekoste iliyoshuka katika A.D. 33. Wape baraka za kipentekoste. Jalia nguvu za Mungu ziingie Kanisani. Jalia kuwepo na karama za uponyaji wa Kiungu zinazopewa Kanisa. Naomba kuwe na wanenaji kwa lugha, mfasiri wa lugha. Jalia kuwe na karama za unabii, na madhihirisho yote mbalimbali; si kujisingizia imani, ama kujaribu kuamini, au kuiga. Jalia iwe halisi, ya kweli, kuja pamoja na Neno, Neno la Mungu likifanywa lijulikane, likitabiri mambo ambayo yanatimia.

268 Wewe ulisema, katika Neno Lako, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye, anayedai kuwa, ama anayedhaniwa kuwa, nabii. Na yale asemayo, basi yasipotimia, msimsikie. Lakini kama yakitimia, basi msikieni nabii huyo, kwa kuwa niko pamoja naye."

269 Mungu, tupe manabii wa aina hiyo. Tupe walio halisi, walio halisi ambao hunena kwa lugha, walio halisi ambao wana tafsiri halisi. Tujalie, Baba.

270 Waponye wagonjwa na wanaoteseka, na ujitambulishe Mwenyewe miongoni mwetu, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari . . .

271 Sasa, ninyi nyote wana wa Mungu Wamethodisti, wana wa Mungu Wabaptisti, nyinyi nyote wana na binti za Mungu, hebu tuinue mikono yetu na kufumba macho yetu, na kumwimbia huu, na kumwabudu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

272 Je, mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wote wampendao, semeni, "Asifiwe Yesu!" ["Asifiwe Yesu!"] Hebu tuliseme tena. "Asifiwe Yesu!" Loo, jinsi mimi . . . Hmm!

273 Katika Kiafrikana, ingekuwa, "Prys die Lord! Jesus, Jesus, Jesus," wanamwita. "Prys Jesus! Dankie, Jesus! Asante Yesu!" Loo, jamani! Ni siku ya jinsi gani! Naam. A-ha. Jinsi—jinsi ninavyosifu, jinsi tunavyomshukuru Bwana mwema kwa ajili ya ninii Yako . . .

Nampenda . . .

274 Mwabuduni tu. Ujumbe mgumu, unaokatakata, namna hiyo. Hebu tuabudu tu. Upendo, utamu wa Roho, kurudi.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Damu ya thamani ya Mwana wa Mungu Mwenyewe imeokoa na kutakasa
Watu wa ajabu kwa ajili ya Jina Lake nao wanaitwa Bibi-arusi.
Ingawa wanadharauliwa na kutwezwa hapa, siku moja Bwana ataleta
Hao waliochaguliwa ndani ya lango, na hilo linastahili kila kitu.

Sote pamoja.

Tukiwa ndani ya malango ya lulu,
Tutajifunza mambo mengi,
Tutakuwa na kinubi kilichotengenezwa kwa dhahabu,
Labda chenye nyuzi elfu moja;
Tutaimba na kupaza sauti na kuchezacheza, (Haleluya!)
Mwana-kondoo atapangusa machozi yetu;
Tutakuwa na juma moja kuu la kurudi nyumbani,
Miaka elfu kumi ya kwanza.

275 Tupe sauti ifaayo kwenye hicho. Hebu tuuimbe tena. Hivi hamuupendi huo? Wazieni tu.

Damu ya thamani ya Mwana wa Mungu Mwenyewe, imeokoa na kutakasa
Watu wa ajabu kwa ajili ya Jina Lake nao wanaitwa Bibi-arusi Wake. (Amina.)
Ingawa wanadharauliwa na kutwezwa hapa, siku moja Bwana atawaleta
wateule Wake ndani ya lango, na hiyo inastahili kila kitu.

Sote kwa pamoja sasa.

Tukiwa ndani ya malango ya lulu,
Tutajifunza jambo kwa wingi,
Tutakuwa na kinubi kilichotengenezwa kwa dhahabu,
Labda chenye nyuzi elfu moja;
Tutaimba na kupaza sauti na kuchezacheza,
Mwana-kondoo atapangusa machozi yetu;
Tutakuwa na juma moja kuu la kurudi nyumbani,
Mwaka elfu kumi ya kwanza.

Hebu tupeane mikono huku tukiimba huo.

Damu ya thamani ya Mwana wa Mungu Mwenyewe, imeokoa na kutakasa
Watu wa ajabu kwa ajili ya Jina Lake nao wanaitwa Bibi-arusi Wake.
Ingawa wamedharauliwa na kutwezwa hapa, siku moja Bwana wetu ataleta
wapendwa Wake ndani ya lango, na hiyo inastahili kila kitu.

Sasa hebu tumwinulie mikono yetu.

Tukiwa ndani ya malango ya lulu,
Tutajifunza mambo mengi,
Tutakuwa na kinubi kilichotengenezwa kwa dhahabu,
Labda chenye nyuzi elfu moja;
Tutaimba na kupaza sauti na kuchezacheza,
Mwana-kondoo atapangusa machozi yetu;
Tutakuwa na juma moja kuu la kurudi nyumbani,
Mwaka elfu kumi ya kwanza.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Kwani alinipenda kwanza.

Sitamwacha kamwe,
Sitamwacha kamwe,
Sitamwacha kamwe,
Kwani alinipenda kwanza.

276 Sitamwacha kamwe, kwa sababu Yeye huniwakilisha. Amina. Yeye ni Mwokozi wangu, na kwa sababu kwamba alikufa kwa ajili yangu. Mimi sistahili. Lakini kwa sababu Yeye alinichukua kama Wake, alifanyika mimi ili niweze kufanyika Yeye. Alifanyika mwenye dhambi na kuchukua dhambi zangu, ili niweze kuwa mwana wa Mungu.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
Loo . . .

277 Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya huyu dada. Na kumpa afya, Bwana, kwa ajili ya utukufu Wako, katika Jina la Yesu.

> . . . mpenda Yesu
> Kwani alinipenda kwanza.

278 Hivi nyimbo hizo za kale haziwafanyii jambo fulani? Ninaikumbuka maskini familia ya watu weusi iliyokuwa ikipiga kambi hapa juu, mwanaume, mke wake, msichana mdogo. Sasa hebu tu . . . Si—si—siwezi kuuimba, lakini nitaujaribu, ninamhisi Roho Mtakatifu juu yangu. Amina. Kasema:

> Loo, ni upendo wa thamani jinsi gani ambao Baba
> Alikuwa nao kwa ajili ya jamii ya Adamu iliyoanguka,
> Akamtoa Mwanawe wa pekee kuteswa
> Na kutukomboa kwa neema Yake.

Loo, napenda hilo!

> Loo, ni upendo wa thamani jinsi gani ambao Baba
> Alikuwa nao kwa ajili ya jamii ya Adamu iliyoanguka,
> Akatoa Mwanawe wa pekee kuteswa
> Na kutukomboa kwa neema Yake.

279 Napenda hilo, nanyi je? Si kuna jambo kulihusu? Sasa, Jumbe hizo ni ngumu, tena kali, na zinakata. Hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo, kali kuliko upanga ukatao kuwili. Lakini yote yakiisha, unaona, Roho Mtakatifu mkuu ameketi humu jengoni mahali fulani, akichunga. Malaika! Loo! Basi, baada ya yote kwisha, tunamwona akinyosha mkono Wake, nazo baraka zinaanza kushuka. Tunainua mikono yetu Kwake, na kumwabudu Yeye katika utamu wa Roho Mtakatifu. Si linawafanyia jambo fulani? Linakusafisha tu, linakupa mwanzo mpya, linakurudisha kwenye Neno.

280 Ni wangapi walio wagonjwa sasa? Semeni, "Naja kuponywa, asubuhi ya leo. Hii ndiyo saa ya kuponywa kwangu."

281 Moja, mbili, tatu, nne, tano, yapata wanane ama kumi wenu. Vema. Sijui kama watoto wangu wadogo hapa wangenifanyia jambo fulani. Mtafanya hivyo? Sijui kama nyote mngerudi tu moja kwa moja huku juu, kidogo tu sasa. Nitawaombeni nyote mshuke chini moja kwa moja kwenye madhabahu hapa, huku tukiomba, huku tungali tunaimba, hebu wale wanaopaswa kupakwa mafuta na kuombewa. Ndugu Neville, njoo. Basi tutawaombea, halafu tuwe na ubatizo wa maji. Na kisha kufumukana rasmi, katika yapata—yapata dakika mbili ama tatu, yapata kumi, ikizidi, nadhani. Vema.

Loo, ni upendo wa thamani ambao Baba
Alikuwa nao kwa ajili ya jamii ya Adamu iliyoanguka,
Akamtoa Mwanawe wa pekee kuteswa
Na kutukomboa kwa neema Yake.

282 Ikiwa mtu yeyote anajua mahali maskini familia hiyo ya watu weusi ilipo, laiti wangalikuja na kuimba huo tena, kwa ajili yangu, wakati wa uamsho. Ilikuwa ni huko chini Broadway, mahali fulani. Ninasahau jina lao; mume, na mke wake, msichana mdogo. Walikuwa na kituo kidogo ndani yake, mwajua, unapofanya hivyo.

Loo, ni upendo wa thamani jinsi gani ambao Baba
Alikuwa nao kwa ajili ya jamii ya Adamu iliyoanguka,
Akamtoa Mwanawe wa pekee kuteswa
Na kutukomboa kwa neema Yake.

283 Mnaona ni kitu gani? Jamii ya Adamu iliyoanguka, ikachanganywa, kote kote. Alishuka chini moja kwa moja kuendelea, kutoka kwa imani halisi ya kiroho, katika Neno la Mungu; kufikia kujuana kimwili, kufikia namna zote za uchafu, kufikia sehemu iliyo duni kabisa.

Na, loo, ni upendo wa thamani jinsi gani ambao Baba
Aliwapa jamii ya Adamu iliyoanguka,
Akamtoa Mwanawe wa pekee kuteswa.

284 Akashuka kufikia kiwango cha chini zaidi kilichokuwapo, na kutukomboa kuturudisha kwenye Neno Lake, kutukomboa kwa neema Yake.

285 Na sasa, asubuhi ya leo, tunasimama kwa neema Yake, tukisema, "Sisi ni watoto Wake. Tuna haki kupata baraka hizi." Yesu Kristo alikufa, kumponya kila mmoja wenu. Hiyo ni kweli. Aliahidi hilo. Na hapa sisi—sisi tunajua ya kwamba hiyo ni Kweli. Ni wangapi wenu mnaojua hiyo ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi, ni mali yako, ni yako, ni yako.

286 Basi kuna kitu kimoja tu kinachoweza kukuzuia usiipate, hicho ni, Shetani akijaribu kukuambia uongo uliochanganywa.

287 Mungu alisema nini? "Alichubuliwa kwa makosa yetu. Kwa mapigo Yake sisi tulipona." Mnaamini hilo kuwa ni Neno la Mungu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa usimruhusu Shetani kukuambia chochote kingine.

288 Neno la Mungu lilisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Umbali gani? "Ulimwenguni kote." Haujafikiwa bado. "Ulimwenguni kote." Hii ilikuwa iendelee muda gani? "Hadi ukamilifu wa dahari." Kitu gani? "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Tazama, niko

pamoja nanyi, siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Jina Langu, watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka, au kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hilo ni Neno.

289 Sasa weka msingi juu ya Hili. Kila kanuni ya Mungu, kaa moja kwa moja juu Yake. Halafu unafikia mahali, na kusema, "Mungu, nimetubu. Nimebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Nimeitambua Damu. Nimemtambua Mwana wa Mungu. Ninakutambua Wewe, Baba Yangu. Umenibariki na Roho Mtakatifu. Sasa Shetani anajaribu kunisumbua na kunifanya mgonjwa. Naja kwa ujasiri." Amina. Hakuna hukumu. "Nimetunza Neno Lako. Nimekaa hapa, kama Hezekia."

290 Wakati Bwana aliposema, "Ambia . . . Isaya, nenda ukamwambie, 'hatatoka kwenye kitanda hicho. Atakufa.'"

291 Akasema, "Bwana, nimetembea mbele Zako, kwa moyo mkamilifu. Ninahitaji miaka kumi na mitano zaidi."

292 Bwana akamwambia nabii, "Rudi, ukamwambie nimemsikia. Ataishi." Hiyo ni kweli. Hubadilisha mambo. Hivyo ndivyo inavyokupasa kuja. Bila hukumu. Kukiwapo na hukumu, unaninii tu . . . una—unapigana tu na hewa. Inakubidi kuja mahali ulipo safi na wazi, "Ninaamini hilo. Ninasimama hapa. Bwana, ninaamini hilo." Kama mimi . . . Kama wewe ni mwenye dhambi, wala humjui Mungu, mwambie Mungu papa hapa, "Bwana, mimi . . . ninataka niponywe. Ninataka kukutumikia. Ila nakupa Wewe, sasa, moyo wangu. Mimi hapa; nitumie mimi."

293 Kama vile nabii, hekaluni, alivyosema, "Mimi hapa, nitume mimi, Bwana." Ndipo Malaika akachukua kaa la Moto.

294 Sasa, tuko kanisani. Kwenye huduma za kiinjilisti, tunatumia aina ile nyingine ya huduma. Hapa ndani, sisi . . . Biblia ilisema hivyo, kwa ajili ya kanisa, "Kukiweko na mtu mgonjwa miongoni mwenu, na wawaite wazee wa kanisa, wawapake mafuta, na kuwaombea. Maombi ya imani humwokoa mgonjwa." Mnajua hilo, Yakobo 5:14.

295 Ndugu Neville hapa, mchungaji wetu, mtu mwema, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, aliyetumwa na Mungu. Ni wangapi ambao wamemtambua Ndugu Neville akipanda? Hivi mmetambua hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nilimsikia akitoa unabii Jumapili iliyopita, kwa mara ya kwanza. Ni nani angaliwahi kuwazia kwamba mhubiri wa Kimethodisti angeweza kusimama namna hiyo? Lakini wakati Roho Mtakatifu aliposhuka juu yake, jambo fulani lilitukia. Mnaona? Naam. Waliingia moja kwa moja ndani yake, moja kwa moja tu. Mnaona? Ukirudi moja kwa moja kwenye kuzaliwa kunakofaa, basi huna budi kusonga mbele.

296 Ukiweka uhai ndani ya punje ya mahindi, na kuiweka katika hali ifaayo, itakua. Achana tu nayo. Itakua.

297 Hivyo ndivyo ilivyo na Kanisa. Kama kweli mnaweza kurudi kwenye kitu sahihi, mdumu tu hapo, mwendelee kusonga mbele, mwangaza wa jua ufaao na maji, na sifa na haleluya, na nyimbo na kadhalika. Kitaleta hili. Kitalileta moja kwa moja, kufikia mahali ambapo mnaweza kufikia na kushika, "Yote yawezekana kwao waaminio."

298 Sasa, wakati anapokupaka mafuta, nitaweka mikono juu yako. Sasa, kwanza, nitaombea kila mmoja wenu. Nami ninawatakeni, kwenye mstari, mwekeane mikono nyinyi kwa nyinyi. Sasa, weakeneni tu mikono nyinyi kwa nyinyi. Ni kwa nini ninafanya hivyo?

299 Sasa, Biblia kamwe haikusema, "Kama Ndugu Branham akikuwekea mikono."

300 Kasema, "Ishara hizi zitafuatana na *hao* waaminio. *Wakiweka* mikono *yao*. . . " Hiyo ni kweli? "Wakiweka mikono *yao*." Mikono yako ni sawa tu na mikono yoyote mingine. Unaona? Hata hivyo, ni mikono ya Mungu inayojalisha. Na, hivyo basi, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

301 Sasa huku mmewekeana mikono, hebu tuinamishe vichwa vyetu. Ninawatakeni nyote, kanisa huko nje, waombeeni hawa.

302 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe msururu huu mkubwa wa watu wagonjwa. Mungu, wazia tu, wengi wa hawa hapa. . .Ninatumaini ya kwamba kila mmoja wao ni watoto Wako, waliozaliwa kwa Roho, wakaoshwa katika Damu, wakajazwa na Roho Mtakatifu, tayari kwa ajili ya kule Kuja. Naye Shetani hawezi kuwafikia, hivyo, kuwafanya watende dhambi. Hawezi kuwafikia, kuwafanya walitilie shaka Neno Lako, ni uongo. Nao wanaendelea na kufuata, kwa makini kabisa. Lakini hata hivyo yeye hujaribu kuja, kuitesa miili yao, kwa sababu anajua ya kwamba miili yao ingali dhambi. Bali nafsi yao imeokoka. Mwili wao hauna budi kurudi mavumbini, bali nafsi yao inaenda kwa Mungu. Kwa hiyo yeye hujaribu kuitesa sehemu hiyo, kile awezacho.

303 Lakini nina furaha sana ya kwamba Wewe ulijumuisha wokovu kwa ajili ya huo mwili, pia. Hii ni—hii ni arabuni ya ufufuo wetu, uponyaji wa miili yetu. Tena, Bwana, kwenye kumbukumbu, leo hii, mamilioni ya nafsi, mamilioni ya miili, ambayo imeponywa. Hivyo basi, tunajua ya kwamba Wewe ni Mungu.

304 Na sasa wamewekeana mikono wao kwa wao. Waangalie, Bwana. Mmoja anamjali mwenzake. Mmoja anataka kujua, pasipo kujali kwamba ni wa kanisa lipi, ni ushirika gani walio nao, kwamba ni wa rangi gani, ama ni kanuni gani ya imani wao. . .Hayo hayana uhusiano wowote nalo, Bwana. Wao ni

watoto Wako. Baadhi yao ni Methodisti, wengine ni wa Baptisti, wengine ni wa Presbiteri, labda wengine ni Wakatoliki. Sijui. Wengine ni Wapentekoste. Lakini Wewe—Wewe huwajui kwa jina hilo. Unawajua kama Wako. Wamenunuliwa kwa Damu. Nao wamesimama hapa, wakiliamini Neno. Nao wanakuja kwa ujasiri. Nami nina—ninasihi kwa ajili yao, kama mtumishi Wako. Mungu, jalia kusiwe na mtu mmoja dhaifu katika jengo hili, ibada itakapomalizika. Wajalie, kila mmoja, aponywe.

305 Wakati mzee Wako aliyepakwa mafuta anapoenenda, akitia hayo mafuta, maskini mafuta hayo yanayoshuka chini juu ya vipaji vya nyuso zao, ambayo yanawakilisha (mafuta ni) Roho. Tunaweka hayo hapo juu, kuwafanya watu wajue ya kwamba mafuta haya safi ya mzeituni yamewekwa juu ya vipaji vya uso wao kwa kufananisha kuja kwa Roho Mtakatifu. Ndipo wakati nikiwawekea mikono, mimi mwenyewe, jalia waende kwenye kiti chao wakiwa na furaha sana, wakishangilia, kazi iliyomalizika. "Yote yamekwisha." Wamepona. Wanaenda nyumbani, wapate afya. Tujalie, Bwana.

306 Na makelele na sifa zitapaa juu, kutoka kote mjini, kote katika sehemu mbalimbali ambako watu hawa watakakokwenda. "Unajua, wakati mmoja nilikuwa na shida ya tumbo, lakini imeisha. Wakati mmoja nilikuwa na *hiki-na-hiki*, magonjwa fulani, lakini yamekwisha. Nilisikia tu Ujumbe ule asubuhi ile, 'Kuzaliwa tena kwenye Neno,' nami nikarudi kwenye Neno. Nami ninaliamini Neno, na sasa nimepona." Tujalie, Baba. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

307 Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Ninataka mzee aende mbele. Hebu ninii . . .

308 Teddy, kama utaweza. Baadhi yenu imbeni *Amini Tu,* kadiri tu mwezavyo sasa.

309 Na hebu wale, ambao wamepita, moja kwa moja kwenye kiti chao, tunapowapaka mafuta na kuwaombea! . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, sasa mimi . . .?. . .

310 Baba uliye Mbinguni, ninapoweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu, mafuta ya upako yangali juu yake . . .

*Hukumu Kwa Uwakilishi* SWA60-1113
(Condemnation By Representation)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 13 Novemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org